

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA PILI

Kikao cha Tisa – Tarehe 12 Februari, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa, tukae; Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Maswali; tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Busega, sasa aulize swali lake.

Kwa niaba yake Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Simiyu.

Na. 114

Hitaji la Vifaa Tiba – Hospitali ya Wilaya Busega

MHE. ESTHER L. MIDIMU K.n.y. MHE. SIMON S. LUSENGEKILE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka vifaa katika Hospitali ya Wilaya ya Busega ili huduma bora za afya ziendelee kutolewa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Busega kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Busega ni miongoni mwa hospitali 67 za Halmashauri zilizoanza kujengwa mwaka 2018/2019 kwa kupewa fedha kiasi cha shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya ujenzi wa majengo saba ambayo ni jengo la utawala, jengo la wagonjwa wa nje, jengo la maabara, jengo la mionzi, jengo la wazazi, jengo la kufulia na jengo la kuhifadha dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 33.5 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa hospitali 67 za Halmashauri ikiwemo Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Busega ambayo imetengewa shilingi milioni 500.

Vilevile katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 33.5 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba katika hospitali 67 za Halmashauri ikiwemo Hospitali ya Halmashauri ya Busega ambayo imetengewa shilingi milioni 500.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa naipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kutupatia pesa shilingi bilioni 5.4 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya ya Bariadi, *Bariadi DC*, Itilima na Busega. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize swali la nyongeza; kwa kuwa tuna upungufu mkubwa wa watumishi katika hospitali zetu hizo za Wilaya nilizozitaja, je, ni lini Serikali itatuletea watumishi wa kutosha hasa madaktari bingwa wa magonjwa ya wanawake? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ujenzi wa miundombinu ya hospitali, vituo vya afya na zahanati, Serikali imeweka mkakati ambao tayari umeanza kutekelezwa wa kuajiri watumishi wa kada za afya kuanzia madaktari na wauguzi na ajira hizi zinatolewa kwa awamu. Lengo la ajira hizi ni kwenda kuhakikisha majengo yote yaliyojengwa yanatoa huduma bora za afya kama ilivyotarajiwa.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hilo ni kipaumbele cha Serikali na itaendelea kuajiri wataalam wa afya kadri ya upatikanaji wa fedha ili kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi katika Halmashauri za Mkoa wa Simiyu na nchini kote.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Olelekaita, swali la nyongeza.

MHE. EDWARD K. OLELEKAITA: Nakushukuru, kwa kuwa swali lililoulizwa linafanana kabisa na matatizo na changamoto tunayopata kama Wilaya ya Kiteto, hususan Hospitali ya Wilaya, tuna upungufu wa mashine ya *x-ray*, jenereta ni mbovu, majengo, gari la kubeba wagonjwa, vitanda na mashine ya usingizi. Ni lini sasa Serikali itapeleka vifaa hivi katika Hospitali yetu ya Wilaya ya Kiteto?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Olelekaita, Mbunge wa Kiteto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ya utoaji wa huduma za afya yakiwemo majengo, vifaatiba, *x-ray*, *ultra sound* na vifaa tiba vingine ni vifaa ambavyo vimepewa kipaumbele katika vituo vyetu vya huduma ili kuweza kufikisha huduma bora kwa wananchi na ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimeeleza jinsi ambavyo Serikali imetenga fedha kiasi cha takribani bilioni 33.5 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali zetu 67 za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba azma ya Serikali ni kuhakikisha tunaendelea kuboresha upatikanaji wa vifaa tiba katika vituo vyetu vyote ikiwemo Hospitali ya Halmashauri ya Kiteto.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tunapozungumzia Hospitali ya Wilaya hatuzungumzii majengo bali tunazungumzia huduma inayotolewa kulingana na *level* ya Wilaya. Ninapenda kujua Serikali ni lini itatuletea watumishi wa kutosha pamoja na vifaatiba katika Hospitali ya Wilaya ya Nkasi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshaji wa miundombinu na watumishi katika vituo na hospitali zetu za Halmashauri ni kipaumbele cha Serikali na utekelezaji wake unafanyika kwa awamu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha na ndiyo maana katika mipango ya Serikali ya kila mwaka Serikali inatenga fedha, kwanza, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaajiri watumishi ili kuondoa changamoto ya watumishi katika hospitali na vituo vyetu. Lakini pili, tunatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaboresha upatikanaji wa huduma bora za afya katika vituo vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua sana kwamba majengo ni kitu kingine na huduma bora ni kitu muhimu pia na ndiyo maana tumeendelea kuboresha miundombinu hiyo, lakini upatikanaji wa vifaa tiba pamoja na watumishi na tutaendelea kuhakikisha kwamba tunatekeleza suala hilo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 115

Mikopo ya Asilimia 10 Toka kwenye Halmashauri

MHE. ZAYTUN S. SWAI aliuliza:-

Kutokana na changamoto za vyanzo vya mapato hususan katika Halmashauri zilizo nje ya miji kumekuwa na uwiano usio sawa wa utoaji wa mikopo.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutafuta njia ya kuweka uwiano sawa wa mikopo hiyo bila kujali mapato ya Halmashauri husika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri hutolewa kwa kuzingatia kifungu cha 37A cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 na Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu za mwaka 2019. Halmashauri inatakiwa kutenga na kutoa asilimia 10 ya fedha za makusanyo ya ndani katika kipindi husika kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu baada ya kuondoa vyanzo lindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa sheria hii ni asilimia 10 ya mapato yanayokusanywa kwenye Halmashauri husika ambayo yanatofautiana kati ya halmashauri moja na nyingine kutokana na fursa zilizopo. Hivyo, kiwango cha mikopo inayotolewa kinategemea uwezo wa makusanyo wa Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu umeendelea kuimarika mwaka hadi mwaka hususan baada ya kuwepo kwa sheria ambapo mikopo imeongezeka kutoka shilingi bilioni 26.1 mwaka 2017/2018 hadi shilingi bilioni 42.06 mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo Serikali inatambua changamoto zinazotokana na utaratibu huu na itaendelea kuuboresha ili kuongeza tija na kufikia malengo ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia mikopo hii.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

MHE. ZAYTUN S. SWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, natambua kwamba Serikali inafanya jitihada kubwa sana kupunguza umaskini vijijini; na kwenye vijiji vyetu vingi vyanzo vya mapato ni vidogo na hivyo kusababisha mikopo ya halmashauri kuwa midogo vijijini ukilinganisha na mijini. Je, Serikali haioni kama kuna haja ya kutafuta njia sahihi ya kugawa mikopo hii ili basi kutimiza dhima hii ya Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; akina mama wa Arusha Mjini wamenituma, sasa hivi kuna sintofahamu ya kugawa mikopo katika Wilaya ya Arusha Mjini. Wanalazimishwa waanzishe viwanda vidogo vidogo ndipo wapate mikopo ya Halmashauri. Akinamama wa Arusha Mjini ni akinamama hodari sana na wanajishughulisha na shughuli nyingi zikiwemo kilimo, ufugaji na hata utalii, wanauza vinyago na shanga na shughuli zingine kadhalika. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu jambo hili?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba halmashauri zetu zinatofautiana uwezo wa ukusanyaji wa mapato na hasa Halmashauri za mijini ikilinganishwa na Halmashauri za vijijini. Ni lengo la Serikali kuwawezesha wajasiriamali wa vikundi tajwa kwa maana ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni jambo ambalo linahitaji tafakari ya karibu zaidi kuona uwezekano wa kuweka kiwango sawa kwa Halmashauri zote kwa sababu pia halmashauri hizi idadi ya wananchi inatofautiana. Unaweza ukatafakari kwa mfano tukisema tuweke kiasi sawa kwa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kwa mfano kwa idadi ya wananchi waliopo na Halmashauri ya Wilaya ya Ileje kwa mfano kwa idadi ya wananchi waliopo. Ni dhahiri kwamba Manispaa na Majiji na Miji zina idadi kubwa zaidi ya wananchi na hivyo ni rahisi kuwa na vikundi vingi zaidi kuliko vijijini.

Kwa hiyo, mgawanyo unaotolewa kwa asilimia 10 ya mapato ni *equitable* inategemeana pia na makusanyo, lakini pia hata idadi ya wananchi katika maeneo hayo inatofautiana. Lakini ni jambo muhimu, tunalichukua na tutaendelea kulifanyia kazi kuona namna bora zaidi ya kuboresha ili wananchi hawa waweze kupata faida ambayo imekusudiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na sintofahamu ya mikopo Arusha Mjini, ninaomba nitoe ufafanuzi kwamba lengo la mikopo ya asilimia 10 ni kuwawezesha makundi hayo katika shughuli zao za ujasiriamali na maelekezo yaliyotolewa ni wao kuunda vikundi hivyo, lakini pia kutafuta shughuli za ujasiriamali ambazo zinawaingizia mapato na kusajiliwa ili waweze kupata mikopo hii.

Kwa hiyo, hakuna utaratibu wa kulazimisha vikundi vya wanawake, vijana au watu wenye ulemavu kufanya shughuli maalum ili waweze kupata mikopo na ninaomba niendeleo kusisitiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia utaratibu na kanuni za utoaji wa mikopo bila kulazimisha wajasiriamali. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa majibu ya Serikali yameeleza bayana kwamba uwiano wa mapato katika kila Halmashauri ni tofauti na hata wingi wa watu ni tofauti; na kwa kuwa shida hii ya mikopo ya akinamama bado inaonekana ni kubwa; je, ni lini Serikali itakuwa tayari sasa kuongeza asilimia ya mikopo kwa akinamama kutoka asilimia nne kwenda asilimia 10? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna uwiano tofauti wa mapato ya ndani ya Halmashauri, lakini hoja ya kuongeza kiwango cha ukopeshaji kutoka asilimia 10 kwenda juu zaidi ni jambo ambalo linahitaji kufanyiwa tathmini na kuona uwezekano wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majukumu haya ya asilimia 10, ikumbukwe pia mapato ya Halmashauri yanahitajika pia kuboresha miundombinu mbalimbali kama ujenzi wa vituo, ukarabati wa madarasa, ujenzi wa madarasa na huduma mbalimbali za wananchi. Kwa hiyo, ni jambo ambalo linahitaji pia kufanyiwa tathmini kuweza kuona faida zake na kuweza uona namna gani litaboresha huduma kwa ujumla katika halmashauri na katika vikundi hivi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niseme tunachukua wazo la Mheshimiwa Mbunge, tutalifanyia

tafakuri na kuona njia bora zaidi ya kuboresha mfumo huu wa utoaji wa mikopo ya asilimia 10. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Noah Lemburis, swali la nyongeza.

MHE. NOAH L. S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nia ya mfuko huo ni kujaribu kusaidia vijana na akina mama na watu wenye ulemavu katika kukuza ajira, hawaoni sasa ni muda mwafaka wa kuongeza muda kutoka miaka 18 hadi 45 badala ya 18 mpaka 35 ambayo hiyo inawazuia wananchi walio wengi kupata mikopo hiyo na kufanya biashara? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Noah kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la mikopo hii kwa vijana ni kuhakikisha kwamba pia inawawezesha kiuchumi, na hasa vijana wa umri wa miaka 18 hadi 35 kwa maana ya *definition* ya kijana. Kwa hiyo, wazo lake la kuongeza wigo kutoka miaka 18 hadi 45 linahitaji pia kulifanyia tathmini na kuona kama miaka 45 iko ndani ya umri wa ujana au kama maana yenyewe ya vijana inahitaji kuboreshwa ili kuongeza wigo huo. Kwa hiyo, ni wazo zuri, lengo ni kuboresha na sisi Serikali tunaomba tulichukue hilo tukalitafakari na kuona uwezekano wa kulitekeleza kwa manufaa ya jamii yetu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ukweli Halmashauri za Tanzania hazilingani upande wa vyanzo vya mapato, na kwa kuwa Halmashauri kama ya Wilaya ya Same vyanzo vya mapato ni vya chini mno, kwa hiyo, inasababisha wananchi wa Wilaya yetu wa Same kuwa maskini ukilinganisha na kwenye Wilaya nyingine ambazo wana vyanzo vikubwa vya mapato.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutafuta taratibu nzuri ya kufanya zile Halmashauri ambazo vyanzo vya mapato viko chini mno nao wakaongezewa ili wananchi wa Tanzania wawe katika uwiano unaolingana? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti ya kiwango cha mapato katika Halmashauri inatokana na wigo wa ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri husika na kimsingi asilimia kumi kama ambavyo jibu la msingi limeeleza, linatokana na mapato ya ndani baada ya kutolewa vyanzo lindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali inaona umuhimu wa kuona namna gani tunaweka mazingira mazuri zaidi kwa Halmashauri zile ambazo zina mapato ya chini zaidi, lakini jambo hili linahitaji kulfanyia tathmini, kulipitia na kuona njia nzuri zaidi ya kuendelea kuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue wazo la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kuweza kuona ni namna gani tunafanya ili tuweze kuboresha huduma hizi za mikopo ya asilimia 10. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, sasa aulize swali lake. Kwa niaba ya Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mheshimiwa Fletei Massay.

Na. 116

Kugawa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu

MHE. FLATEI G. MASSAY (K.n.y. MHE. ZACHARIA P. ISSAAY) aliuliza:-

Mwaka 2015 Serikali ilitangaza kugawa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu na kupitia vikao vya Mabaraza ya Madiwani wa Halmashauri za Mbulu Wilaya na Mbulu Mji walipitisha rasmi mgawanyo wa rasilimali na madeni.

Je, ni lini Serikali itarejesha tamko la mapendekezo hayo ili kufanikisha maendeleo ya mambo yaliyopendekezwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu kupitia vikao vya Mabaraza ya Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu na Halmashauri ya Mji Mbulu waliridhia na kupitisha mgawanyo wa rasilimali na madeni na kuwasilisha mgawanyo huo Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Tarehe 9 Novemba, 2018 mgawanyo wa mali na madeni ya Halmashauri hizo ulitolewa na Waziri mwenye dhamana na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Toleo Namba 45 la

mwaka 2018 pamoja na mgawanyo wa mali na madeni wa Halmashauri nyingine 42 kupitia Tangazo la Serikali Namba 696 la mwaka 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa rasilimali watu, magari, pikipiki, rasilimali na madeni umefanyika kwa asilimia 100 kwa kuzingatia Mwongozo wa Ugawaji wa Mali na Madeni ulioandaliwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI wa mwaka 2014. Katika mgawanyo huo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu (Halmashauri mama) ilipata asilimia 60 na Halmashauri ya Mji wa Mbulu ilipata asilimia 40.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninalo swali la nyongeza.

Kwa kuwa asilimia hizi zipo kisheria na bado kuna ukakasi katika mgawanyo huu; je, yupo tayari sasa kuja kuona uhalisia wa suala lenyewe katika Jimbo la Mbulu Mji na Vijijini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, niko tayari kushirikiana naye na Halmashauri ya Mbulu kuweza kuona namna gani tunatatua huo ukakasi ambao Mheshimiwa Mbunge ameuri pota uliotokana na mgawanyo wa mali kati ya Halmashauri ya Mbulu Vijijini na Halmashauri ya Mbulu Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie kwamba baada ya Mkutano huu wa Bunge tutapanga tuone utaratibu mzuri wa kuwaza kutatua changamoto hiyo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nadhani mmeliona swali. Mheshimiwa Cecil Mwambe, kwako kuna tatizo la mgawanyo? Karibu kwa swali la nyongeza.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ambalo liko kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu linafanana kidogo na suala ambalo liko kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwa maana ya majimbo ya Lulindi pamoja na Jimbo la Ndanda; na kwamba hata mipaka ya kijiografia haijakaa vizuri kiasi kwamba watu wanafikiri kwamba kuna umbali mrefu sana kutoka Makao Makuu ya Jimbo hadi kufika Halmashauri ya Wilaya.

Je, Serikali haioni haja sasa ili kuondoa matatizo kama haya huko baadae, kuona majimbo haya yanaweza kuwa *amalgamated* yakakaa sehemu mmoja kwa maana ya kwenda Masasi Mji?

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, swali la msingi linahusu mgawanyo wa mali. Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Mwambe ataleta hilo kama swali la msingi.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela, sasa aulize swali lake.

Na. 117

Migogoro wa Ardhi Kati ya Hifadhi ya Pori la Akiba Uwanda na Vijiji Vinavyozunguka

MHE. DEUS C. SANGU aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro wa ardhi uliopo katika vijiji vinavyozunguka Hifadhi ya Pori la Akiba la Uwanda?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Jimbo la Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Pori la Akiba Uwanda lenye ukubwa wa kilometa za mraba 5,000 lilianzishwa mwaka 1959 na kutangazwa upya kwa Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Na.12 ya mwaka 1974 kwa Tangazo la Serikali Na. 275 la tarehe 8/11/1974. Tangu mwaka 1974 hadi 2013 pori hilo lilikuwa likisimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na lilikabidhiwa rasmi kwa Wizara ya Maliasili na Utalii tarehe 20/01/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, pori hilo linapakana na vijiji 11 kama ifuatavyo; kuna Kijiji cha Ilambo, Kilyamatundu, Mkusi, Kapenta, Maleza, Kilangawana, Mpande, Legeza, Nankanga C, Liwelyamvula na Kipeta; na vijiji saba ambavyo ni Maleza, Kilangawana, Mpande, Legeza, Nankanga C, Liwelyamvula na Kipeta, ndivyo vyenye mgogoro na Pori la Akiba Uwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia mgogoro huo, orodha ya vijiji husika iliwasilishwa kwa Kamati ya Kitaifa ya Migogoro iliyojumuisha Wizara nane. Utekelezaji wa ripoti ya utatuzi wa migogoro ya ardhi ya Mawaziri nane, chini ya Uenyekiti wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, utaleta ufumbuzi wa mgogoro huu na migogoro mingine kama huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, tunaomba Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela, pamoja na Watanzania wote tuwe na subira wakati utekelezaji wa ufumbuzi wa migogoro hii unaratibiwa. Naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Deus Clement Sangu, swali la nyongeza.

MHE. DEUS C. SANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; katika operesheni za askari wa Wanyamapori kumekuwa na tabia ya askari kunyang'anya wananchi mali ikiwemo mashine za boti, mikokoteni na mali nyingine za wananchi. Nataka kujua kauli ya Serikali ni nini kwa sababu askari hawa wamekuwa wakizikamata hizo mali, wanakuwa nazo zaidi ya miaka miwili mpaka mitatu, ambayo hiyo ni hasara kwa Serikali na kwa wananchi kuwasababishia umaskini?

Swali la pili; naomba kutokana na unyeti wa tatizo hili na hali kuwa tete katika maeneo haya; je, Naibu Waziri yuko tayari kama Wizara kuja baada ya Bunge hili ili wajionee uhalisia wa jambo hili?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya kisheria yanapokuwa yako chini ya kimahakama, sisi kama wahifadhi tunategemea zaidi Mahakama jinsi itakavyoamua. Kwa hiyo, ushahidi mara nyingi lazima ubaki kama kielelezo tosha pale ambapo kesi inapopelekwa Mahakamani, basi ushahidi utolewe ukionyesha na vitu ambavyo amekamatwa navyo mtuhumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala hili, kwa kuwa mhimili wa Mahakama ni sehemu nyingine tofauti na mhimili wa Wizara ya Maliasili na Utalii, hivyo kwenye masuala ya kisheria tunayaacha yanaendeshwa kisheria na vifaa vyote ambavyo amekamatwa navyo mtuhumiwa inakuwa kama ushahidi, hivyo vinaendelea kutumika mpaka pale ambapo Mahakama inakuwa imeshatoa maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lingine la kuamba na Mbunge, Wizara iko tayari na tutaenda kuangalia hiyo migogoro iliyoko katika eneo hilo na tutalisuluhisha kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mmesimama wengi hapo! Hapa nitamchagua ambaye hajauliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Pallangyo, swali la nyongeza.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona na mimi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizoko kule Kwela, zinafanana sana na kule Arumeru Mashariki hususan Kitongoji cha Momela ambacho kimepakana na Hifadhi ya *Arusha National Park*.

Je, Serikali inasemaje kuhusu ule mgogoro ambao umedumu kwa miaka kama mitano sasa hivi, wananchi walikuwa wanaishi kwenye yale mashamba, baada ya ukomo wa umiliki kumalizika, baadae wakaja kuondolewa kwa nguvu?

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimesema awali kwamba Serikali kwa kutambua umuhimu wa wananchi wake na jinsi ambavyo kumekuwa na migogoro ya ardhi hasa upande wa mipaka ya hifadhi, ilitewa Kamati ya Mawaziri nane ambao walitembelea maeneo yote ya hifadhi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii tayari imeshamaliza mchakato wake na tumeshaanza kukaa kwa ajili ya kuangalia namna ya kutatua migogoro hii. Namwomba Mheshimiwa Dkt. Pallangyo awe na subira maana Kamati hii tayari imeshaanza kazi na baada ya Bunge

lako tukufu hili utekelezaji wake sasa utanza. Kwa hiyo, sehemu zote ambazo zina migogoro ya mipaka inaenda kutatuliwa na pale ambapo kuna migogoro mipya itakayoibuka, basi Serikali itaona ni utaratibu gani mwingine ambao itafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe tu rai kwa maeneo mengi nchini ambayo yanakutana na hii changamoto ya mipaka na migogoro ya hifadhi, mara nyingi kumekuwa na tatizo kubwa sana la wananchi kuvamia maeneo ya hifadhi. Maeneo haya kwa asilimia kubwa ni njia za wanyama (shoroba). Kwa hiyo, migogoro mingi tunaanzisha kwa maana ya wananchi kupewa maeneo, lakini kwa upande wa pili tena tunaanzisha mgogoro mwingine wa wanyama wakali kupambana na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, tuwe na hiyo tahadhari pia kwamba tunapokuwa tunayaachia maeneo, lakini tunakuwa tumeanzisha mgogoro mwingine tena kati ya wanyama na binadamu. Maana wanyama siku zote wanapita maeneo yale yale ambayo walizaliwa nayo mwanzo na waliwaacha mabibi na mababu zao pale. Kwa hiyo, hili tatizo litaendelea kuwepo tu kama wananchi wenyewe hawatakuwahi uhifadhi ubaki kuwa hifadhi na maeneo mengine ya wananchi yaendeleo kutumika kwa wananchi wa kawaida. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 118

Hitaji la Ofisi za TRA – Tunduru Kusini

MHE. DAIMU I. MPAKATE aliuliza:-

Jimbo la Tunduru Kusini limepakana na nchi ya Msumbiji kwa upande wa Kusini.

Je, ni lini Serikali itafungua Ofisi za Mamlaka ya Mapato (*TRA*) Lukumbule?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Tunduru Kusini kwa kutambua umuhimu wa kulipa kodi na hivyo kuhitaji huduma za kikodi zisogezwe karibu yao. Ni dhamira ya Serikali kutumia fursa kama hii kusogezwa karibu huduma za kikodi kwa wananchi ili kurahisisha ulipaji na ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) inao utaratibu wa kupitia na kufanya tathmini ya sehemu zote ambazo zinaweza kujengwa ofisi kwa ajili ya kurahisisha ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu unazingatia uwiano wa gharama za ukusanyaji wa mapato na kiwango cha kodi kinachotarajiwa kukusanywa pindi ofisi hizo zitakapofunguliwa kutokana na shughuli mbalimbali za kiuchumi katika eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mwenendo wa kukua kwa biashara kati ya Tanzania na Msumbiji, *TRA* inapenda kuwahakikishia wananchi wa Jimbo la Tunduru Kusini kuwa imelichukua suala hili na itaifanyia kazi kwa kutuma timu ya wataalam ili kufanya tathmini ya kina na endapo kiwango cha kodi kinachotarajiwa kukusanywa kitakuwa kikubwa ikilinganishwa na gharama za ukusanyaji

wa mapato, ujenzi wa ofisi katika eneo hilo utaanza haraka iwezekanavyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini Lukumbule ni lango kubwa ambalo wafanyabiashara wanapita kupeleka bidhaa zao Msumbiji na wale wanaotoka Msumbiji wanapita Lukumbule kuleta Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imekubali kufanya tathmini na kwa kuwa wananchi wa Tanzania wanaopeleka bidhaa Msumbiji mara nyingi hunyang'anywa mali zao kwa kukosa documents za kusafirisha mizigo yao kwenda Msumbiji.

Je, Serikali haioni haja ya haraka kufanya tathmini hiyo ili kuhakikisha wananchi wetu wa Tanzania wanaoenda Msumbiji hawanyang'anywi mali zao mara kwa mara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa Jimbo la Tunduru Kusini lina miji mitano mikubwa; Nalasi, Mchoteka, Malumba, Lukumbule pamoja na Misechela ambayo ina wafanyabiashara wengi na miji hiyo iko zaidi ya kilometa 80 kutoka ilipo Ofisi ya TRA Tunduru Mjini.

Je, Serikali haioni haja ya kupeleka *agencies* katika maeneo hayo ili wafanyabiashara wale waweze kulipa kodi zao wakiwa katika maeneo yao ya biashara? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeona umuhimu wa ushauri wa Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, ushauri tumeupokea na

tutafanyia kazi kwa mujibu wa sheria na miongozo iliyowekwa na pale tutakapopata majibu basi tutamfikishia majibu kwa haraka sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 119

Kuondoa Kodi Kandamizi kwa Wafanyabiashara

MHE. STELLA S. FIYAO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuondoa kodi kandamizi kwa wafanyabiashara na kuweka kodi rafiki ili kuwasaidia kufanya biashara kwa uhuru na kulipa kodi kwa wakati na kuondokana na sintofahamu ya wafanyabiashara kukimbilia kufanya biashara nje ya nchi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mwenaidi Ali Khamisi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Serikali ya Awamu ya Tano haitozi kodi kandamizi. Aidha, Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri ya biashara ikiwa ni pamoja na kuongeza vivutio na fursa mbalimbali za uwekezaji kwa wazawa na wawekezaji kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kupitia na kuimarisha mifumo ya kiseri, kisheria na kitaasisi kwa kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Ufanyaji wa Biashara nchini *(Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment)* wenye lengo la kurahisisha

mazingira ya kufanya biashara ambapo kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2019/2020 ilifuta tozo na ada zisizo rafiki 54 zilizokuwa zinatozwa na wakala, taasisi na mamlaka mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imekuwa ikifanya maboresho mbalimbali kwenye viwango vya kodi kupitia Sheria ya Fedha (*Finance Act*) kila mwaka kwa lengo la kuongeza wigo wa ukusanyaji kodi na mapato mengine ya Serikali, kuchochea ukuaji wa biashara ndogo na za kati pamoja na kuhamasisha uzalishaji viwandani na kulinda viwanda vya ndani dhidi ya ushindani kutoka nje.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, swali la nyongeza.

MHE. STELLA S. FIYAO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri lakini naomba niulize maswali ya nyongeza mawili kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza; ni dhahiri kuwa Taifa letu linahitaji wawekezaji wengi kutoka Mataifa mengine, lakini naamini itakuwa ni ngumu kupata wawekezaji ikiwa hawa tu tulionao wanashindwa kuwekeza kutokana na mrundikano mkubwa wa kodi zilizoko ndani ya Taifa letu.

Sasa nataka kujua je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kulichukua jambo hili na kufanya marekebisho ya sheria za kodi ili wananchi wetu waweze kufanya biashara kwa uhuru? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa *TRA* wamekuwa na utaratibu wa kufanya makadirio ya kodi wanapofika kwenye biashara za watu; ni nini tamko la Serikali katika hili maana *TRA* wamekuwa wakiwakadiria watu kodi kubwa ambazo zinazidi mitaji yao na kusababisha watu wengi kufilisika na kufunga biashara. Ni nini tamko la Serikali kwa hiki kinachoendelea leo? Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mwanaidi Khamisi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Stella Fiyao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kutokana na mazingira mazuri na rafiki hakuna ukandamizaji wa kodi kwa wananchi/wafanyabiashara atakayekimbia kwa kufanya biashara kwa sababu ya kulipa kodi kubwa ambazo Serikali imeziweka kiurafiki na kulipa kodi kwa sheria na utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la pili la Mheshimiwa Stella Fiyao kuwa kama Mheshimiwa anaona kuna kodi kandamizi ambazo wafanyabiashara wanapatiwa basi tungemuomba atuletee changamoto hizo na Serikali itazifanyia kazi kwa mujibu wa sheria na mipango yote iliyowekwa katika Serikali. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Temeke sasa aulize swali lake.

Na. 120

Serikali Irejeshe Eneo la Kurasini EPZ kwa Halmashauri ya Temeke

MHE. DOROTHY G. KILAVE aliuliza:-

Serikali ilitenga eneo la *Kurasini EPZ* tangu mwaka 2014 kwa ajili ya uwekezaji lakini hadi sasa eneo hilo halijaendelezwa kama ilivyokusudiwa.

Je, kwa nini Serikali isirejeshe eneo hilo kwa Halmashauri ya Temeke ili lipangiwe shughuli za maendeleo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dorothy Kilave, Mbunge wa Temeke kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara Serikali kupitia Mamlaka ya *EPZ* ilianza mchakato wa kutwaa ardhi eneo la Kurasini mwaka 2014 kwa madhumuni ya kujenga Kituo cha Biashara na Ugavi wa Vifaa. Hatua mbalimbali za kuendeleza eneo hilo zimefanyika zikiwemo ulipaji wa fidia, kusafisha eneo kwa kubomoa majengo yaliyokuwepo, kufanyika kwa upembuzi yakinifu wa awali na kupatikana kwa hatimiliki. Hatua inayoendelea sasa ni tathmini ya mazingira na maandalizi ya mpango kabambe (*conceptual master plan*) inayofanywa kwa kushirikiana na Bodi ya Kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara katika Bajeti yake ya mwaka 2020/2021 imetenga fedha kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu ya mradi awamu ya kwanza ikiwemo ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la mradi. Tayari Mamlaka ya *EPZ* imeingia mkataba na Kitengo cha Ujenzi cha Jeshi la Kujenga Taifa kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa nia ya Serikali katika kutekeleza mradi huu wa kielelezo kwa mujibu wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa iko pale pale na pia nitumie fursa hii kuomba ushirikiano wake na Halmashauri ya Wilaya ya Temeke kwa ujumla ili kufikia azma ya Serikali kupitia uendelezaji wa mradi huu kwa malengo yaliyokusudiwa. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dorothy Kilave swali la nyongeza.

MHE. DOROTHY G. KILAVE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri, lakini

naomba sasa niseme kwamba sasa ni miaka karibu saba tangu mmelitwaa hili eneo.

Je, haiwezekani kwamba mtachukua tena miaka saba kwa ajili ya kulirekebisha na kuweka mpango huo? Niombe basi kama nilivyosema kwamba wananchi wa Temeke tunatamani kujenga shule za sekondari na msingi kwa sababu tunazaliana sana na maeneo mijini sasa hivi hakuna. Niseme tu kwamba tuombe sasa Wizara yako itupe eneo hili ili sisi katika miaka hii ambayo tumeambiwa tujenge shule za sekondari pamoja na msingi basi tuyapate kwa sababu naona mtakwenda tena miaka saba ijayo katika kutengeneza hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; je, Serikali yetu sasa ina mpango gani wa kumalizia fidia kwa wananchi wa maeneo ya jirani karibu na pale ambapo mmetwaa lile eneo lakini yapo maeneo Shimo la Udongo ambapo mlitakiwa kuyatwaa lakini bado hamjalipa fidia. Naomba maswali yangu haya mawili tuweze kujibiwa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, nomba kujibu maswali mawili ya ziada ya Mheshimiwa Dorothy kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimhakikishie hatutachukua miaka saba tena. La pili ni kwamba eneo lile ni karibu kabisa na Bandari ya Dar es Salaam na sisi kama Taifa tumekuwa mara nyingi tukijadiliana namna gani kuifanya bandari yetu kuwa *effective* na *efficient* na ili iweze kuhudumia waagizaji na wasafirishaji wa bidhaa. Itakuwa ni makosa ya kimkakati tukiligeuza eneo ambalo halizidi mita 500 au 1,000 kuligeuza kuwa eneo la shule. Nataka tu nimshauri yeye na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke na Meya wake wa zamani yumo ndani ya Bunge hili ujenzi wa sekondari sio lazima tujenge kwenda..., tuna uwezo wa

kujenga maghorofa kwa hiyo nawashauri Manispaa ya Temeke mjenge shule kwa mfumo wa maghorofa na ninyi mna mapato mengi kuliko Manispaa nyingi katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kuhusu fidia katika eneo lile tumebaki nadhani kaya kama mbili au tatu ambazo hazijamaliziwa fidia katika eneo la Kurasini na wale wananchi hawakuwa tayari, lakini wako katika hatua za mwisho kumalizana nao na watalipwa haki yao.

Mpango wa Serikali katika lile eneo, eneo la ukubwa wa ekari 20 tunajenga *The First Agricultural One Stop Centre* ili mazo yetu ya kilimo hasa ya mbogamboga na matunda yaweze kusafiri kupitia Bandari ya Dar es Salaam badala ya sasa yanavyotumika kupitia bandari za nchi zinazotuzunguka.

Kwa hiyo, tunawaombeni sana watu wa Temeke mtuunge mkono kufikia azma hii ili eneo lile liweze kutusaidia kutatua changamoto ya usafirishaji wa mazao na kugeuza kuwa ni *export hub* eneo lile. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 121

Soko la Uhakika kwa Wakulima wa Tumbaku

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA aliuliza: -

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa Tabora kuwa na soko la uhakika la zao la tumbaku?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuruhusu soko huria kwa zao hilo ili wakulima wanufaike?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo mfumo wa sasa wa uuzaji wa tumbaku nchini ni wa soko huria ambao unaruhusu kampuni yoyote yenye sifa kuingia mkataba na mkulima kabla ya uzalishaji wa tumbaku ambapo mkulima anakuwa na uhakika wa soko, ubora na bei ya kuuzia tumbaku yake. Wizara inaendelea kuboresha mfumo huo ili uwe mfumo wa uwazi na kuleta mfumo wa *flow market competition*.

Mheshimiwa Naibu Spika, soko la tumbaku linategemea mahitaji ya dunia. Katika soko la dunia ambapo mahitaji ya tumbaku katika soko la dunia yamekuwa yakishuka kwa wastani wa asilimia sita mpaka saba katikamsimu wa mwaka 2019/2020. Hali hiyo, imetokana na mambo mengine ikiwemo janga la *Corona* na na kampeni ya kidunia ya kupunguza matumizi ya bidhaa za tumbaku. Lakini msimamo wa Serikali ni kuendelea kulijenga soko la tumbaku nchini na kuongeza *transparency* katika soko hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hatua zingine ili kuongeza ushindani katika soko la tumbaku. Serikali imeruhusu kampuni nane za Kitanzania ambazo zimeshiriki katika msimu wa 2019/2020 na katika msimu huu wa 2020/2021 kampuni hizi zimetoa jumla ya mikataba yenye uzito wa jumla ya kilo milioni 17 kati ya hizo kilo milioni 9.7 zitatoka kwa wakulima wa Mkoa wa Tabora kutokana na jitihada hizo za kutafuta masoko. Sasa uzalishaji wa tumbaku katika Mkoa wa Tabora utaongezeka kutoka kilo milioni 16 katika msimu wa mwaka 2019/2020 hadi kufika kilo milioni 32 katika msimu wa mwaka 2020/2021.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, swali la nyongeza.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru; pamoja na majibu ya Serikali naomba kumuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao kuu la biashara katika Mkoa wa Tabora ni tumbaku je, Serikali ina mpango gani wa kufanya mazungumzo na kampuni kubwa za kununua tumbaku ili kuweza kuongeza kilo zaidi wakulima wengi waweze kupata manufaa na kilimo hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia wakulima wa Mkoa wa Tabora ili waweze kulima kilimo cha kisasa na waweze kupata zao bora la tumbaku ambalo linaweza kununuliwa katika soko la dunia? Nashukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hawa Mwaifunga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Serikali imekuwa ikichukua jitihada za kuongea na kampuni mbalimbali za ndani na nje na ni vizuri Waheshimiwa Wabunge wakaelewa. Ni hatari sana kama nchi kuruhusu sekta kama ya tumbaku kuwa *dominated* na kampuni za nje peke yake. Hatua ya kwanza tuliyoichukua kama Serikali kwa mara ya kwanza tumeruhusu ushiriki wa kampuni za Kitanzania katika kununua tumbaku na tunazisaidia kupitia Balozi zetu za nje kuya-*connect* moja kwa moja na masoko ya Kimataifa. Sasa tuna kampuni nane ambazo zimeingia katika msimu uliopita na wamenunua tumbaku ya zaidi ya bilioni 12 kutoka kwa wakulima na wamekuwa na baadhi ya changamoto ambazo Serikali imekuwa ikiwasaidia. Lakini jitihada za kuongea na kampuni kubwa duniani, tuna maongezi na kampuni ya *British American Tobacco*, ambayo tunaendelea nayo maongezi. Tunajadiliana nao mfumo wa wao kuingia sokoni. Wao ombi walilolileta Serikalini ni kutaka kununua

kupitia kampuni zilizoko hapa hapa za wenzao za nje na sisi hilo tumewazuia kwa sababu ita-*restrict competition*. Tunawataka waende moja kwa moja sokoni kushindana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubora nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kati ya wakulima wanaofuata *best practice* za kilimo katika nchi hii ni wakulima wa tumbaku na wakulima wa tumbaku wa Mkoa wa Tabora na mikoa mingine hasa Mbeya maeneo ya Chunya wanajitahidi sana kufuata utaratibu mzuri na hatua hii imesababisha hadi kupunguza madaraja ya mazao mabovu. Tumefuta madaraja kumi kwa sababu ya wakulima kufuata *best practice*. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba ubora wa tumbaku ya Tanzania hauna mashaka katika soko la dunia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kunti Majala swali la nyongeza.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Changamoto ya soko la tumbaku inafanana kabisa na changamoto kubwa inayowapata wananchi wa Wilaya ya Chemba kwa soko la mbaazi pamoja na ufuta.

Je, ni lini Serikali itahakikisha wakulima wa Wilaya ya Chemba na maeneo yote Tanzania wanapata soko la uhakika kwa mazao ya mbaazi pamoja na ufuta? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kunti kama ifuatavyo kw aniaba ya Waziri wa Kilimo:-

Kwanza nikiri katika kipindi cha mwaka mmoja, miwili iliyopita soko la mbaazi limekumbwa na changamoto. Sio sisi tu Tanzania peke yake bali nchi nyingi zinazozalisha mbaazi duniani na hii ilitokana na *restriction* iliyowekwa na nchi ya India. Lakini hatua iliyochukuliwa na Serikali, ni kufanya mazungumzo na hivi karibuni katika msimu ujao wa mbaazi

restriction iliyokuwa imewekwa na India itakuwa imeondoka na tutakuwa na uhakika wa kuuza mbaazi katika nchi ya India. Mazungumzo yanaendelea na majadiliano yanaendelea. Nitamkaribisha Mheshimiwa Mbunge na baadhi ya Wabunge mwezi ujao tutakapokuwa na kikao cha wadau wa mbaazi, ufuta, choroko na dengu hapa Dodoma, Mwenyezi Mungu akijaalia kujadili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la ufuta, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali. Biashara ya mazao ni biashara ambayo kidogo ni *complex*, mkulima anapozalisha anapokuwa hana taarifa ya soko ndiyo maana Serikali sasa hivi tumeanza kutumia mfumo wa *TMX* kwa ajili ya *price discovery* na hii itatusaidia sana kuweza kupata *the real value* ya mazao ya kilimo na sasa hivi *commodity market exchange* yetu imeanza majadiliano na *commodity market exchange* za dunia. Kuna maongezi yanaendelea kati ya *commodity market exchange* ya Tanzania na *commodity market exchange* ya India na vile vile tumeanza maongezi na nchi ya China ili tuweze kufungua masoko haya na hatua zinaendelea kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka ujao wa fedha Tanzania tutafungua *the first display* ya mazao yetu ya kilimo. Wizara ya Kilimo. tutaleta bajeti hapa ili Bunge lituidhinishie kufungua *display* ya mazao ya kilimo katika nchi ya China ili wafanyabiashara wetu wawe na eneo ambalo wana *display* mazao yao na kutafuta masoko moja kwa moja. Hii ni hatua ambayo tunachukua. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza kwa kifupi.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Tatizo kubwa la masoko ya tumbaku linafanana kabisa na tatizo la soko la korosho, lakini mimi nimegundua tatizo hili linasababishwa zaidi na kuwepo kwa mdudu mmoja anaitwa Vyama vya Ushirika. Vyama vya Ushirika vimekuwa vikiyumbisha sana masoko kwa wakulima wetu.

Je, Serikali iko tayari kuleta sheria ya Vyama vya Ushirika ili kuvifanyia marekebisho kuondoa matatizo yaliyoko kwenye vyama hivi? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kuchauka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko tayari kuleta sheria na tunafanyia mapitio sheria ya ushirika, lakini sio sahihi kufikiri kwamba mfumo wa ushirika ndiyo una haribu mfumo wa kuuza mazao, bali kuna washirika wanaoharibu vitu vya namna hiyo na Serikali imekuwa ikiwachukulia hatua. Lakini suala la sheria tuko kwenye mchakato na tutaiteta Bungeni kuifanyia marekebisho. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 122

Soko la Uhakika Mazao ya Mahindi Maharage na Muhogo

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta soko la uhakika la mazao ya mahindi, maharage na mihogo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kutafutia wakulima masoko ya mazao ya kilimo ikiwemo Serikali yenyewe

kununua mahindi na maharage kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, Bodi ya Mazao Mchanganyiko, kufanya makubaliano ya (*Government to Government*), masoko ya kikanda, pamoja na kuwatafutia wafanyabiashara ambao watanunua mazao ya wakulima moja kwa moja katika masoko ya nchi za nje vilevile kupitia Balozi zetu.

Aidha, Serikali imeendelea kuondoa urasimu katika mifumo ya kutoa vibali vya kusafirisha na Serikali haijafunga mipaka ya kuuza mazao nje ya nchi. Kila mfanyabiashara ambaye atapata soko, Wizara ya Kilimo itaendelea kumsaidia kumpatia vibali vinavyostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2019/2020 Serikali iliiza jumla ya tani 111,846 za mahindi katika nchi za Afrika Mashariki na kati ya hizo Kenya walinunua jumla ya tani 69,000; Uganda tani 19,000; Zambia tani 900; Rwanda tani 13,000; Burundi tani 7,000 na DRC tani 1150. Aidha, sambamba hilo Serikali bado inaendelea kutoa vibali vya kusafirisha mazao nje ya nchi bila ya masharti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwezi Mei hadi Desemba Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula walinunua jumla ya tani 73,000 za mahindi kutoka kwa wakulima na vikundi vya wakulima. Serikali inaendelea kujenga ghala kwa ajili ya kuongeza uwezo wa uhifadhi. Bodi ya Mazao Mchanganyiko imenunua jumla ya tani 24,000 za mahindi kutoka kwa wakulima na vikundi vya wakulima. Aidha, Wizara imeomba kibali kutoka Hazina kwa ajili ya kuruhusu taasisi zake ziweze kuchukua fedha katika taasisi za benki na iweze kununua moja kwa moja mazao kutoka kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kuhamasisha ununuzi wa mazao ya mihogo ambapo kampuni nne za nje ambazo ni *Dar Canton*, *Jielong Holdings*, *TAEPZ* na *EPOCH Agricultural Development Company* zimenunua jumla ya tani 300 za mihogo mikavu kutoka kwa wakulima. Wizara inaendelea kutoa elimu na kanuni za

uzalishaji wa mihogo bora ili iweze kukidhi mahitaji ya masoko ya kimataifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, swali la nyongeza.

MHE. JOSOPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Pamoja majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wetu wakiwemo wanawake na vijana wanatumia nguvu nyingi, wanatumia muda mwingi, lakini pia wanatumia pembejeo ambazo wanakuwa wamezikopa kwenye vikundi mbalimbali. Wanakopa pesa, wananunua mbolea na dawa; na wanapokuwa wamelima na wamevuna wanakosa soko hatimaye wanashindwa kulipa madeni pale walipo kopa pesa.

Je, Serikali ina mpango gani na inachukua hatua gani kuwa inauza mazao nje ya nchi? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Genzabuke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ni mmoja tu kati ya wanunuzi na sisi kama Wizara tumekuwa tukichukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kusaidia Serikali yenyewe ama taasisi, ama wafanyabiashara wa Kitanzania kuuza mazao yetu nje ya nchi. Miongoni mwa hatua kama taasisi za Serikali, mfano Bodi yetu ya Mazao Mchanganyiko sasa hivi inaanza utaratibu wa kufungua mawakala katika nchi za Kongo, DRC na vilevile katika nchi ya Kenya kwa ajili ya kuuza mazao yetu moja kwa moja kupitia mawakala wa upande huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hatua nyingine ambayo tunachukua kama Serikali, ili kuhakikisha wakulima wanapata soko la uhakika ni kuzijengea uwezo taasisi zetu kwa maana ya *NFRA* na *CPB* na ndio maana nimesema katika jibu langu la msingi kwamba, sasahivi tuna mazungumzo na wenzetu wa hazina, ili kuruhusu taasisi zetu hizi mbili ziweze kuchukua fedha katika taasisi za benki na zinunue kama taasisi za kibiashara waweze kuuza mazao mbalimbali, lakini vilevile tunatumia balozi zetu kuwasaidia wafanyabisahara wa kitanzania kuuza mazao yetu yaliyochakatwa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kupitia Bunge hili nataka niwaombe wachakataji wa mazao hasa ya mahindi, hakikisheni mashine zenu mmezifungia kitu kinaitwa *fortification* ili unga wetu uwe unga *fortified* na uweze kumeet *international standards*. Hili ni jambo ambalo linatukwaza katika kuuza mazao nahii ni *peoject* ambayo inatakiwa sekta binafsi waweze kuifanya. Kwa hiyo, Serikali inachukua hatua hizo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, swali la nyongeza.

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la masoko nje ya nchi limeendelea kuwa changamoto hususan baadhi ya bidhaa zetu, kwa mfano parachichi na hivi karibuni tumeona parachichi letu la Tanzania limefika nchi fulani na ikaharibiwa nje ya nchi.

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na masoko haya ya nje ya nchi? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Chana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jitihada zinazofanywa na wenzetu hasa katika nchi zinazotuzunguka hasa nchi kama za *SADC* ku-*sabotage* wafanyabiashara wa Kitanzania kuuza mazao katika nchi zao wakati sisi kama nchi tunaruhusu kwa mujibu wa sheria na mikataba tuiyonayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukio alilolitaja Mheshimiwa Mbunge ni tukio ambalo limetokea katika nchi moja iliyoko Kusini mwa Afrika. Tumeanza mazungumzo na wenzetu wa *Foreign Affairs* na mimi nataka niwahakikishie Wabunge, Tanzania imeshiriki katika ukombozi wa nchi nyingi katika Afrika, hatutaruhusu wafanyabiashara wetu kudhalilishwa kwa njia yoyote ile. Tutachukua hatua dhidi ya nchi hii na sisi tutazuia bidhaa zao pale ambapo itabidi kufanya namna hiyo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Josephat Kandege, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Naomba niulize swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba uwepo wa taasisi kama *NRFA* na Bodi ya Mazao Machanganyiko ni pamoja na ku-*act* kama *price stabilizer*.

Je, ni hatua gani ambayo Serikali imechukua ili chombo hiki kiweze kutoa pesa na uwezo mkubwa ili kinunue mazao kwa wananchi tukijua kabisa kwamba majadiliano ya kupata *guarantee* Serikalini imechukua muda mrefu sana?

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Kandege, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wizara, tumeendelea majadiliano na hazina, lakini vilevile katika kipindi cha hivi karibuni taasisi yetu ya *CPB* imeweza kupata fedha kutoka katika mifuko ya hifadhi ya jamii zaidi ya bilioni saba na fedha hizo wameshaanza kurudisha kwa hiyo, wamekuwa *credible* na wameonesha *proper business plan*. Bado tunaendelea na maongezi na wenzetu wa Hazina na tutapata *solution*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuna maongezi na Benki ya *CRDB* na *NMB* katika ku-*finance* miradi ya *CPB* ya kununua mazao kwa kutumia *collateral management system* badala ya kusubiri kibali kutoka Hazina.

Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mazungumzo yetu yako katika hatua nzuri na tutafikia kule ambako siku zote yeye toka akiwa Kamati ya Bajeti akisukuma tutafika huko Mwenyezi Mungu akijalia hivi karibuni, *Inshallah*. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Bryceson Magessa Tumaini, Mbunge wa Busanda, sasa aulize swali lake.

Na. 123

**Vituo vya Kuongeza kasi ya Maji Mradi wa Maji
Chankorongo – Busanda**

MHE. TUMAINI B. MAGESSA aliuliza:-

Je, ni lini Mradi wa Maji wa Chankorongo utawekewa vituo vya kuongeza kasi ya maji ili upate uwezo wa kutoa huduma katika maeneo mengi zaidi Jimboni Busanda?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer* Maryprisca Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Chankorongu unatumia maji ya Ziwa Victoria ukiwa na pampu yenye uwezo wa kuzalisha lita 155,000 kwa saa ambapo kwa sasa unatoa huduma kwa wakazi wapatao 23,756 wa vijiji vitano vya Chankorongu, Chikobe, Nyakafulo, Chigunga na Kabugozo katika Jimbo la Busanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha mradi huu unanufaisha wakazi wengi wa Jimbo la Busanda, Serikali imeanza upanuzi wa mradi huo wa maji kwa kuanza utekelezaji wa Mradi wa Maji Katoro-Buseresere wenye thamani ya shilingi bilioni 4.2. Kupitia mradi huo wakazi wa vijiji vya Luhuha, Nyakagomba, Inyala na Mji Mdogo wa Katoro watanufaika na huduma ya maji. Kwa sasa utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 20 na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Aprili, 2021.

Aidha, katika kuhakikisha wananchi wengi wananufaika na huduma ya maji, Serikali kupitia programu ya Mpango wa Malipo kwa Matokeo inaendelea na ujenzi wa miradi ya maji ya bomba katika vijiji vya Nyakagwe na Rwamgasa ambapo wakazi wapatao 14,315 wa vijiji hivyo watanufaika na huduma ya maji safi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bryceson Magessa Tumaini swali la nyongeza.

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile mradi huu wa Chankorongu ulioko Ziwa Victoria unaweza tu kupita katika vijiji alivyovitaja; je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba maji kutoka Ziwa Victoria yanaweza kufika kwenye

maeneo ya Nyarugusu, Bukoli na Kata ya Nyakamwaga?
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Magessa, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa eneo la Nyarugusu, maeneo ya machimbo haya Serikali tayari tuko kwenye mpango wa kupitisha mradi mkubwa pale wa maji kutoka Geita na utapita eneo hilo maji yanayotoka Ziwa Victoria na eneo lile pia, watapata *extension* kwa maana ya mtandao wa mabomba, maji yatafikia hapo na vilevile nipende kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge namna ambavyo waliweza kuzungumza na Mheshimiwa Waziri alipokuwa ziara katika eneo lake, basi yale mazungumzo yamezingatiwa kama ambavyo umeona tayari Meneja yule aliweza kubadilishwa na sasa hivi yupo Meneja mwingine ambaye yupo tayari kuendana na kasi ya Wizara hivyo, eneo la Nyarugusu pia litapata maji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea, swali la nyongeza.

MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya maji ya Busanda inafanana kabisa na changamoto ya maji iliyoko Korogwe Mjini. Nimekuwa nikifuatilia kwa Mheshimiwa Waziri na ameniahidi tatizo la Korogwe litatatuliwa na mradi wa miji 28 ambao Korogwe ni sehemu ya mradi huo.

Je, Serikali inawaahidi vipi wananchi wa Korogwe kwamba lini mradi huu utatekelezwa ili kuweza kutatua

changamoto ya maji ambayo inawakabili wananchi wa Korogwe Mjini?

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, *Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea, Mbunge wa Korogwe Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipende kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu amekuwa ni mfuatiliaji mzuri na nimeshaweza kuongea naye mara kadhaa na kumhakikishia eneo lake kupata maji na uzuri Korogwe Mjini ipo ndani ya ile miji 28 ambayo fedha tayari zipo na muendelezo wa maandalizi unaendelea na hivi karibuni kuanzia mwezi Aprili miji ile 28 shughuli za kupeleka maji zinakwenda kuanza mara moja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mtemvu swali la nyongeza.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mradi huu wa Busanda unafanana sana na ule mradi uliopo Wilaya ya Ubungo, hasa mradi wa *2f2b*, unaoanzia Changanyikeni, Chuo Kikuu mpaka Bagamoyo na hasa ujenzi wa tanki kubwa la lita milioni sita pale Tegeta A, Kata ya Goba. Je, mradi huu utakamilika lini ili wananchi wote wa Kata ya Goba wapate maji safi, salama na yenye kutosheleza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, *Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtemvu kutoka Kibamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi yote hii ambayo tayari utekezaji wake unaendelea Wizara tunasimamia mikataba na namna ambavyo mkataba unamtaka yule mkandarasi kukamilisha mradi ule. Mheshimiwa Mbunge ninakupa uhakika kwamba tutasimamia kwa karibu na mradi ule utakamilika ndani ya muda ambao tumeupanga.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, swali la nyongeza.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mradi wa maji wa Wilaya ya Muleba ambao unalenga kusaidia kata sita ambao umefanyiwa usanifu tangu mwaka 2018. Je, Wizara itaujenga lini na utakamilika lini kwa ajili ya kuwahudumia wakazi wa Wilaya ya Muleba?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, *Engineer* Maryprisca Mahundi, majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daktari, Mbunge kutoka Muleba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ambao usanifu wake umekamilika nao tayari Wizara tunaendelea na michakato kuona kwamba mradi huu tunakuja kuutekeleza ndani ya wakati.

Waheshimiwa Wabunge pale tunaposema kwamba, maji ni uhai, Wizara tunasimamia kuhakikisha kuona kwamba, wananchi wote wanaenda kupata maji safi na salama ya kutosheleza kwa lengo la kulinda uhai wa wananchi. Hivyo, Mheshimiwa Daktari nikuhakikishie kwamba, namna usanifu umekwenda vizuri na utekezaji wake nao unakuja vizuri namna hiyo.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa, sasa aulize swali lake.

Na. 124

Tatizo la Maji Mpwapwa

MHE. GEORGE N. MALIMA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo la muda mrefu la uhaba wa maji kwa wananchi wa Mji wa Mpwapwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, *Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua tatizo la muda mrefu la uhaba wa maji katika mji wa Mpwapwa. Katika kutatua tatizo hilo, mikakati ya muda mfupi na muda mrefu imekuwa ikitekelezwa. Kwa upande wa mikakati ya muda mfupi, mwaka 2020/2021 Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuchimba visima virefu viwili katika eneo la Kikombo. Ujenzi wa bomba kuu kutoka katika visima hivyo viwili mpaka katika tanki la Vingh'awe, kuongeza mtandao wa maji katika maeneo ya pembezoni ambayo ni Vijiji vya Vingh'awe na Behero. Aidha, kazi nyingine itakayofanyika ni kufunga pampu mpya kwenye kisima cha Kikombo ambacho kitaongeza uzalishaji wa maji katika kisima hicho kutoka lita 40,000 kwa saa hadi lita 65,000 kwa saa. Kukamilika kwa kazi hizi kutaboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika mji wa Mpwapwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mpango wa muda mrefu, Serikali kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mpwapwa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji ya Dodoma (*DUWASA*) inaendelea kufanya usanifu

unaotarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2021 na kubainisha maeneo ambayo yana upungufu mkubwa wa maji katika Mji wa Mpwapwa ambapo vitachimbwa visima virefu vinne na kuongeza mtandao wa mabomba katika Mji wa Mpwapwa na viunga vyake. Aidha, katika mwaka 2021/2022, Serikali itakarabati mradi wa maji wa mtiririko wa Mayawile na Kwamdyanga.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa George Natany Malima, swali la nyongeza.

MHE. GEORGE N. MALIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa tatizo la maji katika Mji wa Mpwapwa limekuwa la muda mrefu. Na kwa kuwa, Serikali imekiri kwamba, ni kweli limekuwa la muda mrefu na kwamba, wana mpango wa kuchimba visima viwili katika eneo la Kikombo ili kuongeza upatikanaji wa maji katika mji ule.

Je, ni lini uchimbaji huu wa visima hivi viwili utakamilika ili watu wa Mpwapwa nao wapate unafuu wa shida ya maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; mwezi Januari timu kutoka Wizara ya Maji ilikuja kutembelea katika Jimbo langu, tulikagua miradi miwili ya maji mmoja katika Kijiji cha Vingh'awe na mmoja katika Kijiji cha Manhangu; na mradi ule wa Vingh'awe ulitengenezwa siku nyingi, lakini historia iliyopo ni kwamba ulipochimbwa miundombinu ilijengwa chini ya kiwango; ulifanya kazi siku tatu tu mabomba yalipasuka, lakini tenki ambalo lilijengwa *below standard* pia nalo lilibuja lote halafu ule mradi ulikufa, lakini mradi wa Manhangu pia una *story* inayofanana.

Je, Serikali inasemaje kuhusu hili, maana walikuja kukagua na wakaahidi kwamba wataifanyia matengenezo ili ifanye kazi. Je, ni lini watakuja kurekebisha hiyo miradi miwili?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, *Engineer* Maryprisca Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa George Malima, Mbunge wa Mpwapwa kama ifuatavyo:-

Swali lake la kwanza ni lini mradi ule unakwenda pesa zitapelekwa ili mradi uendeleo kutekelezwa. Jibu lake kwa sababu mradi uko ndani ya mwaka wa fedha huu 2020/2021 Mheshimiwa Mbunge nakuhakikishia kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha kwa maana ya mwezi Juni hii fedha itakuwa imefika na tutasimamia utekelezaji wake kwa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ameongelea kuwa mwezi Januari kuna timu kutoka Wizarani ilikwenda na ni kweli. Miradi hii anayoiongelea ya Vingh'wale pamoja na Manhangu kwa pale Mpwapwa ni kati ya miradi ya ule mpango wa vijiji kumi ambao Wizarani imekuwa ikiifanyia kazi na vijiji hivi kwa hakika vilikuwa na changamoto kubwa sana ya maji, lakini kwa awamu hii sisi tumejipanga kuhakikisha kuona kwamba miradi ile kwenye ile programu ya vijiji kumi tunakwenda kuisimamia ambayo ina vijiji takribani 177 vyote tunakwenda kuhakikisha tunarekebisha pale ambapo kidogo palikuwa na mapungufu. Lakini vilevile tutahakikisha wananchi wetu wanakwenda kupata maji safi na salama na ya kutosheleza.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Shamsia Mtamba, swali la nyongeza

MHE. SHAMSIA A. MTAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianza mpango wa kulipa fidia kwa wananchi wa Mtwara Vijijini waliopitiwa na bomba la maji mwaka 2015; nataka kujua mradi huu umekwamia wapi wakati uthamini ulishaanza kufanyika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji *Engineer* Maryprisca Mahundi, majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika,ahsante kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shamsia kutoka Mtwara Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi ambao umeshafanyiwa usanifu Serikali tumejipanga tunakuja kuhakikisha kuona kwamba usanifu ule unakamilika na utekelezaji wake utakamilika. Miradi yote namna ambavyo ipo kwenye mikataba namna ambavyo tumekuwa tukianza tunakwenda kuhakikisha kwamba maji yanatoka na changamoto zote ambazo zilikuwepo huko nyuma kwa kipindi hiki tunakwenda kuzimaliza.

NAIBU SPIKA:Mheshimiwa Ali Makoa swali la nyongeza

MHE. ALI J. MAKOA:Mheshimiwa Naibu Spika,ahsante sana; kwa kuwa tatizo la Mji wa Mpwapwa linafanana na Mji wa Kondo, Halmashauri ya Mji wa Kondo ina tatizo kubwa la muda mrefu la maji na tatizo ni uchakavu wa miundombinu.

Ni lini Serikali itapeleka fedha kutatua tatizo la miundombinu chakavu ya maji iliyojengwa miaka ya 1970?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji *Engineer* Maryprisca Mahundi, majibu kwa swali hilo

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika,ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Makoa kutoka Kondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi yote ambayo muda wake wa uhai umekwisha kwa maana ya *lifespan* imesha-*expire* sasa hivi tayari tumeshaanza mchakato wa kuona namna gani mwaka ujao wa fedha kukarabati labda kwa

kubadilisha mabomba kama yamechakaa sana au kuongeza mabomba kwa maana ya mtawanyo wa miundombinu au kuona kwamba kama kipenyo kilikuwa kidogo tutaweka mabomba makubwa kulingana na idadi ya watu namna ilivyoongezeka na uhitaji wa maji safi ulivyoongezeka hivyo nipende kumwambia Mheshimiwa Ali Makoja kuwa Kondoa napo tunakwenda kupaletea mapinduzi makubwa kuondoa changamoto ya maji.

NAIBU SPIKA:Ahsante sana tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge sasa aulize swali lake.

Na.125

Ahadi ya Kuboresha Barabara – Nkenge

MHE. FLORENT L. KYOMBO aliuliza:-

Pamoja na kazi nzuri ya miradi ya kutengeneza barabara Nkenge, viongozi wetu kwa nyakati tofauti wameahidi kufanya maboresho ya miundombinu ya barabara za Kabyaile/Shozi – Njiapanda ya Gera, Minziro – Mutukula, Kaja Hospitali ya Mugana (Bwanja).

Je, ni lini barabara hizo zitatengenezwa ili kuondokana na kero hizo zinazowapata wananchi wanaotumia barabara hizo kiuchumi?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mutukula – Minziro (kilometa 15.8) ni barabara ya ulinzi na pia ni moja ya ahadi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Barabara hiyo inatakiwa kufunguliwa na tayari kilometa mbili zipo na

zinatumika. Kilometa 13.8 zilizosalia zinapita katika mashamba na Hifadhi ya Msitu wa Minziro na zitaendelea kufunguliwa kwa awamu. Makisio ya ujenzi wa barabara hiyo yamefanyika na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ambapo jumla ya shilingi bilioni 3.63 zinahitajika kwa ujenzi wa kiwango cha changarawe na shilingi bilioni 9.994 zinahitajika kwa ujenzi wa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zingine ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja, Serikali itaendelea kuziboresha ili kuhakikisha kuwa zinapitika vizuri katika majira yote ya mwaka. Ahsante.

NAIBU SPIKA:Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, swali la nyongeza.

MHE. FLORENT L. KYOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa majibu ya Serikali na nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri na weledi katika masuala yote ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza na swali la kwanza ni barabara ya Katoma - Bukwali ambayo ni barabara inaunganisha nchi yetu nanchi ya Uganda na ni barabara muhimu kwa uchumi kwa wananchi wa kata za Gera, Ishozi, Bwanjai, Kashenye na Kanyigo; barabara hiyo yenye kilometa 39.5 nishukuru Serikali sasa hivi kilometa nne zimeanza kujengwa kwa kiwango cha lami na je ni lini kilometa 35.8 zilizobaki zitawekwa kwenye bajeti na kuweza kukamilishwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili ni barabara ya Bunazi - Nyabiyanga - Kasambya - Kakindo na Minziro ambayo barabara hiyo inaunganisha Makao Makuu ya Wilaya pamoja na nchi yetu ya Uganda lakini kuwa ni barabara kiungo kwa wananchi wote wa Tanzania kila mwezi Januari wananchi wanaenda kuhiji katika eneo takatifu la Mtakatifu Yohana Maria Muzeyi aliyelikwa hapo na ni mojawapo ya mashahidi 22 wa Uganda.

Je, ni lini barabara hiyo yenye kilometa 35.8 na yenyewe itaweza kutengenezwa kwa kiwango cha lami nakushukuru kwa nafasi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja ya Katoma - Bukwali tayari ipo inaendelea kujengwa na kilometa 4.2 kama alivyosema zinajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana na mimi kwamba bado wakandarasi wawili wako *site* wakiwa wanaendelea kufanya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami kwa kilometa ambazo tunaamini kilometa 2.2 zitakamilika mwezi Aprili na Serikali bado inaendelea kutafuta fedha na katika bajeti ijayo barabara hii tunaamini kwamba itapata fedha kuendelea kukamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara alizozitaja zote hizo za vijiji mbalimbali na kata mbalimbali tunatambua kwamba ni muhimu kwa uchumi wa wananchi wa Nkenge na bado Serikali tunaahidi kwamba itaendelea kuzikarabati na pale fedha itakapopatikana kuzijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

NAIBU SPIKA:Ahsante sana Mheshimiwa Condester Sichalwe swali la nyongeza.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa ya kunipa kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ubovu mkubwa wa miundombinu ndani ya Jimbo la Momba. Je, ni lini Serikali itatusaidia kutujengea kilometa 15 za kiwango cha lami kwenye Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Momba katika Kata ya Chitete ikiwa ni sambamba na ahadi ya mama yangu mpendwa Mheshimiwa Makamu wa Rais alipotembelea Jimbo la Momba tarehe 13 Oktoba, 2020 alituhidi angeweza kutusaidia barabara hiyo? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA:Uliza swali.

Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naombakujibuswali la nyongeza la Mheshimiwa Condester Sichalwe, Mbunge wa Momba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ahadi ya Makamu wa Rais wakati wa kampeni ilitolewa mwaka huu wa kampeni 2020; kwa hiyo, kama Serikali ahadi hii tumeichukua na tunaifanyiakazi. Kwa hiyo, katika awamu inayokuja ya bajeti tunategemea kwamba zitakuwa ni kati ya barabara ambazo zitategewa fedha na *once* zikitengewa fedha barabara hiyo itajengwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph George Kakunda swali la nyongeza

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii, naomba niulize Serikali na wananchi wa Sikonge wanasikiliza na Mkoa wa Tabora; je, baada ya kuwa Serikali imekamilisha maandalizi yote ya ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya Ipole - Lungwa yamekamilika usanifu kila kitu. Je, sasa bado fedha na mkandarasi Serikali itaanza lini kujenga barabara hiyo ili kuunganisha Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Tabora?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi engineer Godfrey Kasekenye Msongwe majibu

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakunda, Mbunge wa Sikonge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Ipole - Lungwa ni kati ya barabara zinazounganisha Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Mbeya na kama alivyosema taratibu zote zimekamilika, kinachotegemewa tu ni lini itatangazwa kwa sababu sasa hivi tuko kwenye maandalizi ya manunuzi kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na kama alivyosema wananchi wake wanamsikia ni barabara muhimu inayounganisha na mkoa na mkoa, kwa hiyo ninahakika barabara hii itatengewa bajeti na taratibu za manunuzi *once* zikikamilika basi tutakuwa tumepata mkandarasi na itanza kutekelezwa, ahsante.

NAIBU SPIKA: Wizara ya Nishati Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo sasa aulize swali lake.

Na. 126

Hitaji la Umeme wa REA - Vitongoji vya Namtumbo

MHE. VITA R. KAWAWA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza umeme wa REA kwenye baadhi ya vitongoji vya vijiji vya Namtumbo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme nchini (*TANESCO*) pamoja na Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) inaendelea kupeleka umeme katika vijiji na vitongoji nchini. Vijiji vyote 14 vilivyobaki katika Wilaya ya

Namtumbo vitapatiwa umeme kupitia Mradi wa REA Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili unaotarajiwa kuanza mwezi Februari, 2021 na kukamilika mwezi Septemba, 2022. Mradi huu utahusisha pia kupelekea umeme vitongoji vya vijiji vitakavyopelekewa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa vitongoji vyote nchini vikiwemo vya Wilaya ya Namtumbo vitaendelea kupelekewa umeme kupitia miradi ya umeme vijijini kulingana na upatikanaji wa fedha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, swali la nyongeza

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwanza naomba niipongeze Serikali Kuu kwa kazi nzuri inayoifanya ya kutusambazia umeme. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wa Namtumbo nyumba zao na taasisi wamefanyakazi yao nzuri ya *wiring*, lakini wanacheleweshewa kuunganishiwa umeme hususan kijiji cha Mbimbi na Taasisi ya *Hunger Seminary* na Shule ya Sekondari ya Msindo.

Je, Serikali inaweza kuelekeza *TANESCO* waharakishe uunganishwaji wa umeme katika vijiji na taasisi hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mazingira ya Namtumbo maeneo mengi yana mchwa na yanasumbua sana nguzo za umeme zisizokuwa *treated* vizuri. Je, Serikali inaweza kuelekeza namna bora ya ku-*treat* nguzo zinazowekwa au kuwekwa nguzo rafiki na mazingira ya mchwa ya Namtumbo na kwingineko ili kuepuka hasara inayoweza kujitokeza katika mradi huu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Byabato Stephen Rujwahuka, majibu

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Namtumbo ni mojawapo ya Wilaya ambazo zilikuwa zinapelekewa umeme katika awamu ya tatu mzunguko wa kwanza wa *REA*. Kilichotokea ni kwamba baada ya kufanyika kwa kazi ya awali wakandarasi waliowengi waliongezewa kazi za nyongeza katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuwafikia wananchi walio wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Namtumbo imekuwa ni mojawapo kati ya maeneo ambayo yameongezewa maeneo ya nyongeza na hivyo kushindwa kukamilisha kazi iliyopangwa kwa wakati. Mkandarasi ambaye alikuwa anafanyakazi katika Mkoa wa Ruvuma *NAMIS Cooperate* ameongezewa muda wa kukamilisha kazi katika mkoa huo mpaka kufikia mwezi Aprili na katika Wilaya ya Namtumbo tayari ile kazi iliyokuwa imeongezeka nguzo zimesimikwa, waya zimepelekwa na kilichobaki sasa ni upatikanaji wa mita kuweza kuwafikishia huduma wale wote waliopelekwa umeme. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nimuahidi Mheshimiwa Vita kwamba ifikapo mwezi Aprili tayari wale wote waliounganishiwa umeme watakuwa wamewashiwa umeme katika maeneo yao bila kuchelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la pili alitaka kujua uwezekano wa kuweka miundombinu itakayokuwa rafiki na ya uhakika katika maeneo ambayo tayari yana matatizo mbalimbali. Tunafahamu na sasa ni maelekezo ya Wizara kwamba katika yale maeneo ambayo oevu kwa maana ni maeneo yenye majimaji, katika maeneo ya hifadhi na katika maeneo yenye matatizo mengine na changamoto kama hizo za miti kuliwa na mchwa tumeelekeza kwamba wenzetu wa *TANESCO* na *REA* basi watumie nguzo za zege

zinaitwa *concrete polls* ili kuhakikisha kwamba tukiziweka basi zinakuwa za kudumu na zinakaa kwa muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niongezee kwamba kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wanayafahamu maeneo yao yana matatizo gani, basi maelekezo ya Wizara ni kwamba wale wakandarasi watakaoenda kufanyakazi katika Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili wa *REA* wahakikishe wanawasiliana pamoja na mamlaka nyingine watakazoziona kwa maana ya *TANESCO* kupeleka kwa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya lakini pia wafanye *consultation* kwa Waheshimiwa Wabunge ili waweze kutoa maoni yao na ushauri wao maeneo gani yanaweza yakafanyiwa nini hata kama siyo ya kitaalam lakini yakichanganywa na ya kitaalam yatatusaidia kuhakikisha miundombinu yetu inadumu katika maeneo husika. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, swali la nyongeza.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona naomba niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa changamoto zilizoko Namtumbo zinafanana kabisa na changamoto zilizoko Mkalama hasa Kata ya Mwanga ambayo haikuwahi kupata umeme kabisa katika awamu zote. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu kata hii ambayo imekuwa ikiutizama tu umeme huu wa *REA* katika kata nyingine?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Byabato Stephen Rujwahuka majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Mkalama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyokwisha sema kwamba katika Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili wa *REA*, tutapeleka umeme katika vijiji vyote Tanzania vilivyobaki bila

kupata umeme ambavyo hesabu yake ilikuwa ni 2,150. Kazi hiyo itaanza mwezi huu wa pili na tunahakikisha kwamba kufika mwezi Septemba, 2022 vijiji vyote vilivyopo nchini Tanzania vitakuwa vimepata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongezee kwamba tunapopeleka umeme vijijini, kimsingi tunapeleka kwenye Mkoa, Wilaya, Kata, vijiji halafu Vitongoji. Kwa hiyo, kuna vitongoji ambavyo pia vitanufaika na awamu ya tatu, mzunguko wa pili wa upelekaji wa umeme kwenye mradi huo ambao utaanza mwezi huu na kukamilika kufikia mwezi Septemba, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge wa Mkalama kwamba vijiji hivyo vilivyopo katika kata hiyo, vitapatiwa umeme kwa uhakika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, swali la nyongeza.

MHE. ENG. MWANAISHA ULENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu Serikali inatekeleza Mpango wa *peri-urban* kuhakikisha vijiji vilivyopo ndani ya majiji navyo vinapatiwa umeme. Naomba kujua ni lini Serikali itaweka wazi ratiba yake ili na vijiji vilivyopo ndani ya Jiji la Tanga vitapelekewa umeme huo wa *REA*? Nashukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanaisha, Mbunge wa Tanga kwa kueleza kwanza kidogo kwamba Serikali yetu kupitia maelekezo yanayotolewa na Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, imekuwa ikipeleka umeme katika maeneo mbalimbali kwa taratibu tofauti tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao Wakala wa Umeme *TANESCO* ambao una jukumu na wajibu wa kuhakikisha wanapeleka umeme katika maeneo yote ya mjini na vijijini kwa maana ya kwamba ile miradi inayowekwa katika mazingira fulani, ikishakamilika, basi *TANESCO* wanaendelea kupeleka umeme katika maeneo hayo. Hata hivyo, tumekuwa na hizo *REA I*, *REA II* na *REA III*; pia tumekuwa na kitu kinaitwa *densification* (Mradi wa Umeme Jazilizi); vile vile iko hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameisema ya *peri-urban* ambao ni mradi unaopeleka umeme katika maeneo ya mijini lakini yenye asili au uonekano wa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa *peri-urban* ulianza kwa kupeleka umeme katika Majiji ya Arusha, Mwanza, Dar es Salaam, Mbeya na Dodoma na awamu ya kwanza imeelekea kukamilika, itakamilika mwezi wa nne mwaka huu na baada ya hapo sasa tutaingia katika awamu ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba awamu ya pili itakapoanza basi Waheshimiwa Wabunge wote watafahamishwa na wale wote ambao ni wanufaika watapata nafasi hiyo. Pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo ya *peri-urban* bado yanapelekewa umeme na Wakala wa Umeme *TANESCO* kwa kuzingatia kwamba ni jukumu lake kuhakikisha kwamba anapeleka umeme katika mazingira yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kuwa taarifa itapatikana na ratiba kamili itafahamika. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Kalenga hasa Vijiji vya Wangama, Lupembelwasenga pamoja na Welu kwa kutaja tu vichache tayari walishaunganisha umeme,

walishalipia na walishafanya *wiring* lakini hawajawashiwa umeme mpaka sasa.

Je, Serikali inatoa kauli gani ili wananchi hao waweze kuwashiwa umeme wao? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Byabato Stephen Rujwahuka, majibu.

Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Kalemani, majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri katika maswali ya nyongeza. Vilevile nawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kuuliza maswali ya msingi sana katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wateja wote ambao wameshafanya malipo na wanasubiri kuunganishiwa umeme pamoja na wateja wote ambao wameshafanyiwa *survey*, lakini wanasubiri kuunganishiwa umeme, tumetoa muda wa miezi mitatu wateja wote wawe wameshaunganishiwa umeme nchi nzima. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Mbunge wa Kalenga kwa kuuliza swali hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ili kuharakisha shughuli za kuwaunganishia umeme wateja nchi nzima, tumebadilisha mpango wa wataalam wetu kusubiri magari, badala yake *TANESCO* itawanunulia magari ma-*surveyor* wote na ma-*technician* ili wawahi kuwaunganishia umeme wananchi, ndani ya muda uliokusudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongeze kidogo kuhusiana na suala la maeneo ambayo ni ya mijini; kulingana na swali ninalojibu ambalo Naibu Waziri amejibu vizuri, lakini niongezee kidogo. Iko mitaa mingi ambayo iko karibu na miji na vijijini hasa katika maeneo ambayo ni ya Majiji na Manispaa, likiwemo Jiji la Mbeya, Iringa, Mwanza, Dodoma hapa, mradi wa *peri-urban* unaendelea na miradi yote katika mitaa 122

itapelekewa umeme ndani ya miezi sita ijayo. Ahsante sana.
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali. Naleta kwenu matangazo kabla hatujaendelea na ratiba iliyoko mbele yetu. Tutaanza na tangazo la wageni walioko hapa Bungeni siku ya leo. Tutaanza na wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Kundi la kwanza ni wageni 26 wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa, ambaye ni Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ambao ni wapiga kura wake na wanafunzi wa *UDOM* wakiongozwa na Ndugu Julieth Kwandikwa. Karibuni sana.
(Makofi)

Huyu Julieth ni mtoto wa Mheshimiwa Kwandikwa ama! Mtoto wa Mheshimiwa Kwandikwa ndio yupi jamani, tuanze kupimana umri humu ndani? (Makofi)

(Hapa mtoto wa Mhe. Elias J. Kwandikwa alisimama akiwa katika jukwaa la wageni)

NAIBU SPIKA: Eeh, karibu sana. Huyu ni binti wa Mheshimiwa Waziri.

Pia tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Ole-Nasha ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambao ni wapiga kura wake kutoka Ngorongoro, Mkoa wa Arusha, nao ni Ndugu Thadeus Clamian, Ndugu Timmoth Ole-Yaile na Ndugu Nailejileji Kambaine. Karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni 55 wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde ambao ni wanafunzi pamoja na walimu kutoka Shule ya Sekondari Viwandani iliyopo Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwalimu Malick Masoud. Karibuni sana.
(Makofi)

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ambao ni Wanachama wa Chama cha Mapinduzi kutoka Mkoa wa Geita wakiongozwa na Mwenyekiti wa Tawi la Katoma, Ndugu Gabriel Lufungulo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile tunao wageni 18 wa Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma ambao ni wanachama wa UVCCM - *SUA* wanaotoka Mkoa wa Manyara na Morogoro wakiongozwa na Ndugu Polkari Saragu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunaye mgeni wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambaye ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Wilaya ya Mbozi Mkoa wa Songwe, Ndugu Mwasiti Shabani. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Hussein Amar ambao ni viongozi wastaafu wa Chama cha Walimu Wilaya ya Nyang'hwale Mkoa wa Geita; na hawa ni Ndugu Charles Luchagula na Ndugu Aloyce Mboje. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni watatu wa Mheshimiwa Tarimba Abbas, ambao ni familia yake kutoka Kinondoni Jijini Dar es Salaam, wanaongozwa na mke wake, Ndugu Latifa Fazel, ameongozana na Ndugu Mohamed Tarimba na Ndugu Talha Tarimba. Karibuni sana. Mke wake asimame; shemeji, wifii. *(Makofi)*

(Hapa mke wa Mhe. Tarimba G. Abbas alisimama akiwa katika jukwaa Wageni)

NAIBU SPIKA: Eeh, Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, msiwe mnalitapita sana hapa kwa Mheshimiwa Tarimba. *(Kicheko)*

Tunao wageni 12 wa Mheshimiwa Maimuna Pathan ambao ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam na rafiki zake ambao ni Mawakili kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na

mume wake Ndugu Jafary Mburussi. Sijui wako upande gani hawa? Nadhani hawajapata fursa ya kuingia. Tutawatangaza wakifika humu ndani. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Agness Mathew Marwa ambao ni wapiga kura wake kutoka Butiana Mkoa wa Mara, nao wanaongozwa na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mazami, Mheshimiwa Mwita Muniko, Ndugu Mwanaisha Gibbe na Mwalimu Godliver Gibbe. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima ambao ni wapiga kura wake kutoka Wazo Kota, Jijini Dar es Salaam na hawa ni Ndugu Grace Pallangyo, Ndugu Wilfred Kaberege na Ndugu Hilda Kasonso. Karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile tunaye mgeni wa Mheshimiwa David Mathayo ambaye ni shemeji yake kutoka Kinondoni Jijini Dar es Salaam na huyu ni Ndugu Emmanuel Shoo. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka ambaye ni Kiongozi wa Diaspora Uingereza, anaitwa Ndugu Prince Katega. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Minza Mjika, ambao ni watoto wake kutoka Mkoa wa Simiyu, Ndugu Mahulu Emmanuel, Ndugu Sunday Mahulu na Ndugu Grace Chalamila. Wamekaa upande gani? Nadhani hawakupata nafasi.

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Cecil Mwambe ambao ni wapiga kura wake kutoka Ndanda, Ndugu Mohamed Nyagali na Ndugu Abdallah Mkundapai. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Abubakari Asenga kutoka Kilombero, Mkoa wa Morogoro ambaye ni mke wake, Mwalimu Amina Rajabu. Yupo upande gani jamani? Eeh, karibu sana. Jamani mmemwona hapo wizi yetu na shemeji

yenu wengine! Mheshimiwa Abubakari Asenga ameoja jamani, tuisogee sogee pale. *(Kicheko/Makofi)*

Wapo pia wageni mbalimbali hapa Bungeni ambao wamekuja kwa ajili ya mafunzo, wageni hao ni watumishi 28 kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Habari na Elimu ya Mpiga kura, Ndugu Monica Mnanka ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wanachuo 60 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma ambao wamekuja hapa Bungeni kujifunza jinsi tunavyoendesha shughuli. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wanachuo 30 kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe ambao wamekuja kwa ajili ya mafunzo pia. Wageni kutoka Mzumbe karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile tunao wanafunzi 65 na walimu watano kutoka Shule ya St. Peter Claver ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake. Wanafunzi kutoka Peter Claver, Karibuni sana. Eh, kuna shule matata jamani, watoto wanavaa suti. Sasa hapa kuna Mbunge jana alikuwa anauliza kuvaa *track suit*, sasa kuna suti. Karibuni sana. *(Kicheko/Makofi)*

Pia tunao wanachuo 40 wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kilichoko Mkoa wa Morogoro ambao ni wanachama wa Chama cha Mapinduzi, nao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia ninalo tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Shally Raymond ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania. Naye anawatangazia Waheshimiwa Wabunge Wanawake wote kwamba leo tarehe 12 Februari, 2021 mara baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge, Waheshimiwa Wabunge Wanawake waelekee *African Dreams Hotel* kutakuwa na

semina ama mafunzo kwa ajili ya Wabunge Wanawake wote. Kwa hiyo, baada ya kuahirisha tu shughuli za Bunge mchana huu Waheshimiwa Wabunge Wanawake tunaalikwa na Mwenyekiti wetu kwamba tuelekee huko. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo niliyonayo. Kwa hiyo, tutaendelea na ratiba iliyoko mbele yetu. Katibu.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria kwa Ajili ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali zipatazo 12 kwa lengo la kuondoa upungufu ambao umejitokeza katika sheria hizo wakati wa utekelezaji kwa baadhi ya masharti katika sheria hizo (*A Bill for an Act to Amend certain Written Laws in order to keep the laws updated with some challenges observed in its implementation*) Kusomwa Mara ya Kwanza; na...

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mwongozo wa Kiti.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI: Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho ya Kihisibu na Wakaguzi wa Hesabu kwa lengo la kuongoa upungufu ambao umebainika wakati wa utekelezaji wa sheria hiyo (*A certain Bill for an Act to amend the accountancy and auditors legislation act in order to address some challenges which were encountered during its implementation*) Kusomwa Mara ya Kwanza.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2021 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.2) Act, 2021*)

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa
Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021
[The Accountants and Auditors (Registration)
(Amendment) Act, 2021]**

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Miswada hii miwili imesomwa kwa mara ya kwanza na kwa utaratibu wetu itapelekwa kwenye Kamati kwa mamlaka aliyonayo Mheshimiwa Spika, ataelekeza Kamati gani iangalie Miswada hii. Kwa hiyo, hapa Bungeni imeshasomwa kwa mara ya kwanza.

Baada ya kusoma Miswada hii kwa mara ya Kwanza, nimwite Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Vijana, Kazi, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, aje atoe hoja ya kutengua Kanuni za Bunge.

HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, VIJANA, KAZI, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu Maelezo ya Hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge chini ya Kanuni ya 34(3) na Kanuni ya 174(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkutano huu wa Pili wa Bunge ulipangwa kukamilika tarehe 12 Februari, 2021 baada ya kukamilisha shughuli zilizokuwa zimepangwa.

Na kwa kuwa tarehe 9 Februari, 2021 Kamati ya Uongozi ilipokea Hati ya Dharura kutoka kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka

2021 kufanyiwa kazi kwa hatua zake zote katika Mkutano huu wa Pili unaoendelea.

Na kwa kuwa katika Kikao chake kilichofanyika siku ya Alhamisi, tarehe 11 Februari, 2021, Kamati ya Uongozi iliazimia kuwa Bunge likutane siku ya Jumamosi tarehe 13 Februari, 2021 ili kushughulikia Muswada huo wa Sheria.

Na kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 34(15) Bunge halifanyi vikao vyake siku za Jumamosi, Jumapili na siku za mapumziko.

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba Kanuni ya 34(2), (4) na (15) itenguliwe kwa mujibu wa Kanuni ya 34(3) na Kanuni ya 174(1) ili kubadili muda wa Vikao vya Bunge na kuwezesha Bunge kukutana Jumamosi kuanzia saa tatu asubuhi na kuendelea na kikao chake hadi saa nane mchana litakapoahirishwa; isipokukwa kwamba katika siku hiyo hatutakuwa na kipindi cha Maswali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge wengi.

Kwa hiyo, sasa nitawahoji kwa utaratibu wetu kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Vijana, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU SPIKA: Tutasubiri kuona mahudhurio, lakini hoja hii imeungwa mkono na Wabunge walio wengi. Kwa hiyo, waliosema ndiyo wameshinda. Kwa hiyo, siku ya Jumamosi kutakuwa na Mkutano wa Bunge. (Makofi)

Katibu. Ah, Katibu kabla hujasema neno, Mheshimiwa Kandege ulisimama kwamba kuna Kanuni imevunjwa humu ndani.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naamini inaweza ikawa imetokea bila kuwa na taarifa sahihi, kwa sababu kwa sasa hivi kuna taarifa ambazo zinazagaa kwenye mitandao kwamba Mheshimiwa Mbunge mwenzetu hatunaye; Mheshimiwa Nditiye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu ambao umewekwa na Bunge lako, sidhani kwamba ni busara kuendelea na hiki ambacho kinaendelea. Naomba Mwongozo wako.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kama mliyomsikia Mheshimiwa Kandege hicho alichokisema ni jambo kubwa zito la kusikitisha, lakini kiti hakina rasmi kuhusu jambo hilo kama alivyosema kwamba zinazagaa, kwa hiyo, kama ni kweli nitaletewa taarifa kwa kuwa sina taarifa siwezi kutoa maamuzi yoyote kwa sasa. Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

KAMATI YA MIPANGO

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Gwajima.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba mwongozo wako kupitia Kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako liko jambo limetokea wakati Serikali inajibu swali namba 123 lililoulizwa na Mbunge

Pindi Chana kwamba pametokea parachichi ya Tanzania imekwenda Afrika ya Kusini tani 25 na imefika Afrika ya Kusini imearibiwa na kutupwa kwenye takataka na mbaya zaidi wamefanya hivyo wakati wana *record* kwenye *YouTube* na kwenye *whatsapp* na kama tunavyojua wanunujaji wengi wa parachichi za Tanzania ni watu wa Scandinavia, Norway, Sweden na wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wanunujaji wa parachichi letu wameona duniani kwamba parachichi yetu inaharibiwa inatupwa kwenye dampo huku wanarekodi wakati nchi hiyo hiyo ya *South Africa apple* zake zinaingia kila siku, na haitoshi pia limetokea la kufanana na hilo kwamba mchele wetu na wafanyabiashara wetu unaosafiri kwenda *South Sudan* umepita kule Uganda na wenyewe umezuwa kwenda. *(Makofi)*

Je, Serikali ina tamko gani kwa kuona bidhaa zetu zinakuwa *sabotage* katika medani ya kibiashara na Bunge letu liko kimya? Naomba unipe juu la tamko la Serikali kwa jambo lililotokea. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ni kweli wakati Mheshimiwa Pindi Chana alipouliza swali yeye hakutaja nchi gani, lakini alisema bidhaa za kutoka hapa nchini kuna nchi ambazo zingine kama zinakataa kama zingine zinaharibu na sasa Mheshimiwa Gwajima na kututajia nchi mahususi ambazo bidhaa za kutoka hapa nchini zimepata huo msukusuko na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri hapa yaliashiria kwamba hiyo taarifa Serikali inayo na kwa kile alichokizungumza hapa amesema wao watachukuwa hatua nchi ambazo zinakataa bidhaa zetu na sisi tutakataa bidhaa zao. *(Makofi)*

Kwa muktadha huo hakuna Kanuni yoyote iliyovunjwa kwa sababu swali lilivyoulizwa na majibu ya Serikali na Serikali imeshatoa msimamo hapa kwamba nchi ambazo hazipokei bidhaa zetu na wao bidhaa zao hatutazipokea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini nadhani ni jambo ambalo kwa sasa limetokea kwenye mazao ya kilimo lakini inaweza kutokea kwenye vitu vingine ni muhimu Serikali ikaangalia namna ambavyo mahusiano yetu na hizi nchi inaweza kuyaweka mazingira ambayo na sisi tusionekane ndiyo wapokeaji kila wakati hata kwa vile vitu ambavyo tunao uwezo na sisi kuonyesha kwamba vyao kama haviji na vyetu visiende, ni utaratibu wa kawaida kama nchi haipokei ya kwetu na wa kwao wasipokelewe. Lazima kama nchi kuweka misimamo ya namna hiyo na ninataka kuamini kwa msimamo waliotoa hapa Naibu Waziri kama msimamo wa Serikali watachukua hatua hizi na sisi tutazona zikichukuliwa hizo hatua. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunatarajia kuanzia sasa kutoka kwenye hizo nchi zilizotajwa na zingineo zilizotajwa Tanzania ichukuwe hatua na dhani wabunge watakuwa wakiona na wao zikichukuliwa hizo hatua. *(Makofi)*
Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kufuatilia hili jambo lililosemwa hapa, kwa hiyo, tukishaletewa taarifa tutafanya utaratibu wetu wa kawaida. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi tuwe na utulivu, tuendeleo kwa sasa wakati tunasubiri taarifa rasmi.

Tutaendelea na wachangiaji wetu na nimeshapata majina hapa ya wachangiaji walioomba kutoka kwenye vyama vyetu vilivyoko hapa Bungeni, tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Tlemei, Mheshimiwa Twaha Mpembenwe ajiandae.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kukishukuru Chama changu cha

Mapinduzi na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano. Kwanza kabisa nitamke tu kwamba naiunga mkono hoja, lakini mimi ni muumini wa uchumi wa soko na ninashukuru kwenye mpango tuliuletewa sura ya tatu unaongelea ushiriki wa sekta binafsi kama chachu ya uchumi shindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo nitaongelea sekta ya kilimo. Kilimo kama tunavyosema ni uti wa mgongo wa nchi hii au Taifa letu, lakini ukiangalia maendeleo ya kilimo chetu hayaoneshi kwa vitendo kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa hili, nikiangalia kwenye mpango wenyewe tumeambiwa kilimo mpaka sasa kinachangia asilimia 27 ya *GDP*, lakini pia kinachangia asilimia 24 ya mauzo nje ya nchi. Nikilinganisha na nchi jirani nchi nyingine ndogo ambazo ukiangalia ukubwa wa Taifa lenyewe wao kilimo kinachangia asilimia 35 ya *GDP* na asilimia 40 ya mauzo nje ya nchi. Tunayo kazi kubwa ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo chetu kimebubikwa na mambo mengi ambayo nadhani katika mpango huu lazima tuyapatie wajibu, mojawapo ya haya matatizo tuliyonayo Taifa letu limekumbwa limekumbwa na ugonjwa wa kanuni na tozo nyingi kwenye sekta hii, kanuni zetu zimekuwa mnyororo zimekuwa *broke* ya kutufanya tusonge mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya yangu ninayotoka zao kubwa tulionalo ni zao kahawa, lakini zao hilo wakulima wanalima, wanajitahidi, wanakwenda kuuza na kanuni tuliyonayo mpaka leo kwamba mkulima akishalima lazima auze kwenye vyama vya msingi/ vyama vya ushirika na anapokwenda kuuza anayo matatizo yake, lakini awezi kulipwa pesa itabidi asubiri mwezi moja, wa pili, wa tatu na wakati mwingine miezi minne, lakini wakati huo huo tunavyo viwanda vinavoongeza thamani ya kawaha.

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba mjadala sasa uahirishwe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kwagilwa.

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 79 inasema; Mbunge anayependa mjadala unaoendelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye anaweza kutoa hoja kwamba mjadala sasa uahirishwe na atataja mjadala huo uarishwe hadi wakati gani pia atalazimika kutoa sababu kwa nini anataka mjadala uarishwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ulizosema zinazagaa tunalo *group* la Wabunge ambalo ni *group* rasmi na huwa tunatumia kwa taarifa rasmi na taarifa hii inayozagaa imetolewa na Naibu Waziri wa Ardhi, kwa hiyo, tuliichukulia kwamba ni taarifa rasmi...

MWENYEKITI: Nimeshakuelewa.

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: ...na mwenzetu aliyefariki hapa mimi ni jirani yangu hapa, kwa hiyo, nashindwa kuendelea...

MWENYEKITI: Nimeshakuelewa.

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nimeeleza jambo hili ni zito, siyo kwamba mimi ni rahisi sana kukaa hapa mbele, hapana. Lakini utaratibu wetu wa kutoa taarifa ni makosa mtu kuandika taarifa ambazo ofisi hajithibitisha. Huyu aliyeandika hapo mimi sijajuwa ni nani amemtuma, kwa sababu Waziri wa Afya yuko hapa ndiyo tunafuatilia huko ili mimi niletewe taarifa kwamba huyu mtu amefariki.

Sasa kila mtu akipata taarifa huko akawa na yeye mtoa taarifa, kila mtu ni msemaji hata kama umepata taarifa sisi wote ni viongozi humu tuwe watulivu, tujue namna ya kupeana taarifa nzito kama hizi zinazotuumiza sisi wote, ni Mbunge mwenzetu, ni kiongozi mwenzetu, tunatamani taarifa isiwe kweli, lakini ikiwa ni kweli basi mimi hapa mbele nasubiri taarifa rasmi. Siwezi kusema kuna mtu ameandika huko na wapi amesema inaniwia vigumu kufanya maamuzi kwa

muktadha huo Wabunge naomba mnielewe nafikiri tumeelewana vizuri.

Tumeshatuma huko ujumbe tunasubiri taarifa rasmi namna ambavyo Bunge linapokea taarifa rasmi. Kwa hiyo, ikija tu hiyo taarifa msiwe na wasiwasi, huyo aliyetoa taarifa sina hata namna siwezi kusema tunamshukuru au tunamshangaa, mimi mwenyewe na ndiyo nipo hapa na mimi ndiyo msaidizi wa Spika na Spika ndiyo msemaji wa Bunge. Sasa aliyetoa taarifa huko ni nani, amepewa na nani, kama alikuwepo hospitali, daktari ndiye aliyemwambia ama amefanyaje.

Waheshimiwa Wabunge, tuwe watulivu nasubiri taarifa, hata mimi/sisi tulioko humu ndani jambo hili ni zito kwa namna hiyo hiyo lazima tuoneshe uongozi hata katika hili. Nadhani tumeelewana Waheshimiwa. Waziri wa Afya yuko hapa naomba awasiliane na Katibu wangu wa Bunge ili nipate taarifa hapa, tusije tukaendelea sana kumbe huyo aliyesema ama huyo aliyeandika anazo taarifa kweli za kutoka hospitali.

Alikuwa anaendelea kuchangia Mheshimiwa Kikoyo.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naongelea zao la kawaha Wilaya Muleba na Mkoa wa Kagera kwa ujumla kwamba kulingana na kanuni tulizonazo kwamba mkulima hawezi kuuza kahawa yake moja kwa moja kwa wafanyabiashara katika mkoa huo, lakini wakati Naibu Waziri wa Kilimo akijibu swali baadhi ya mazao wanaruhusiwa na pale Muleba wapo wafanyabiashara ambao wamewekeza kwenye kusindika zao la kahawa, lakini hawaruhusi kuuza kahawa hiyo moja kwa moja kwenye vile viwanda na kama tunavyofahamu kilimo na viwanda lazima tuvioanishe, matokeo yake wenye viwanda wanalazimika kununua kahawa hiyo kutoka vyama vyetu vya msingi kwa bei ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inayo madhara makubwa sana kwa uchumi, kwanza bidhaa wanayozalisha kutokana

na kupata malighafi kwa bei ya juu haiwezi kushindana kwenye soko, lakini pia wakulima ambao wanauza bidhaa yao kwenye vyama vya msingi hawapati bei nzuri na wakati mwingine inawachukua muda kulipwa pesa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni muda muafaka sasa kuruhusu wafanyabiashara ambao wamewekeza kwenye viwanda ambavyo vinasindika mazao yanayopatikana katika maeneo mahalia badala ya kufungwa na kanuni ambazo zinazorotesha na kuumiza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo taasisi ambazo zinashughulika na masuala ya ushindani, tuziruhusu kampuni binafsi zishindane na vyama vyetu vya ushirika na vyama vyetu vya msingi ili kuleta tija katika masoko yetu na kuhakikisha kwamba wakulima wanapata bei nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine na lamsingi na nzuri tukiwaruhusu wafanyabiashara hao kununua mazao moja kwa moja kutoka kwa wakulima ambao ni zao la kahawa, watahakikisha kwamba wanawapa pesa nzuri lakini pia wanaweza kuwafuatilia wakulima wale kuhakikisha kwamba wanazalisha na wanapatia msaada kuhakikisha kwamba mazao yao na mashamba yao yanakuwa bora muda wote na kilimo kinakuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.
(Makofi)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kama Wabunge wengine walivyokuwa wamesimama hapo, walikuwa wametoa taarifa ambazo nimeshaeleza hapa kwamba Mheshimiwa Spika ndiye msemaji wa Bunge na ndiye anayeweza kuzungumza ama kama si yeye, basi mimi kama msaidizi wake na Kanuni ya 173 huwa inatutaka tufanye hivyo linalotokea jambo zito kama hili. Lakini Mheshimiwa Spika ameniletea ujumbe hapa kwamba yuko kufuatilia uhakika wa hizi taarifa na yeye mwenyewe atakuja hapa kwa ajili ya kutoa taarifa rasmi ya jambo hili.

Kwa hiyo, kwa muktadha huo wakati huu ambao tunamsubiri Mheshimiwa Spika kwanza apate taarifa hiyo rasmi kutoka hospitali yetu ya Benjamin Mkapa, lakini pia aje hapa atueleze ni taarifa hihi ambayo ameipata *either* ya mwenzetu kwamba ametangulia ama taarifa zilizotoka hazikuwa sahihi yeye atakuja kutoa maelezo hapa.

Kwa hiyo wakati huu ambao tunamsubiri Mheshimiwa Spika tutaendelea halafu yeye akishafika basi mimi nitampisha ilia je aseme hizo taarifa zimekaa namna gani.

Waheshimiwa nilikuwa nimentaja Mheshimiwa Daniel Tlemai, Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, kama Mheshimiwa Spika atakuwa ajafika tutaendelea na mwingine.

MHE. DANIEL A. TLEMAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa sababu ni siku yangu ya kwanza kuchangia katika Bunge lako tukufu, lakini vilevile niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Karatu kwa kunichagua kwa kura nyingi na hatimaye nikawa jimbo la Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nikishukuru chama changu Chama cha Mapinduzi kwa kuniamini na mimi kupeperusha bendera na hatimaye nikawa Mbunge wa jimbo la Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme mchango wangu utajikita katika maeneo ya kilimo kama walivyoongea Wabunge walio wengi katika ukumbi huu, lakini vilevile katika jimbo la Karatu sisi ni wakulima, tunalima mazao ya kitunguu, mahindi na mbaazi, lakini ushauri wangu ni nini kwa Serikali na Wabunge walio wengi hapa wameongea kwamba katika eneo hili la kilimo Wabunge wengi wamechangia kwamba suala hili la kilimo kuwekwa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Karatu imetokea mara nyingi sana katika Wizara ya Kilimo kwamba sasa kipindi chakula kikiwa kidogo ndani ya nchi wanasema mazao yetu tusipeleke nchi za nje, lakini wakati huo mkulima

huyo amelima kwa shida, wakati huo mkulima huyo wa Jimbo la Karatu na wa nchi ya Tanzania amelima kwa mikopo ya benki na kila kitu, lakini wakati huo Wizara ya Kilimo inasema tusipeleke mazao yetu nje ya nchi kwa sababu ndani ya nchi hii kuna uhaba wa chakula.

Sasa ninataka kujua, hivi ni kazi ya wakulima wa Tanzania kulisha watu waliokuwa mjini ambao wanakaa kwenye baridi na wakati huo sisi tufanye kazi ya kulisha walioko mjini kwamba sasa tusiuzue mazao yetu nje kana kwamba ndani ya nchi hii ya Tanzania kuna shida ya chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa nini mazao yetu tusiuzue yakaisha kabisa baadae tukaagiza chakula kutoka nje kikaja ndani ya Tanzania kama tunavyoagiza mafuta yanaisha ndani ya nchi hii na baadae tunaagiza nje ya nchi ili kwamba watu wetu waweze kupata pesa katika eneo hili la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo katika Jimbo langu la Karatu tunalima kilimo cha aina mbili; kuna kilimo cha mvua na kuna cha umwagiliaji na sisi pale tuna tarafa nne katika Jimbo la Karatu lakini Tarafa ya Eyasi inalima kilimo cha umwagiliaji lakini tarafa nyingine zinalima kilimo hiki cha mvua na kule kwenye Jimbo langu la Karatu ukiwa unalima kilimo kile cha mvua unaweza kupata gunia tano kwa hekari mpaka gunia kumi, lakini unapolima kilimo kile cha umwagiliaji unaweza kupata gunia 30 mpaka gunia 40. Sasa ushauri wangu ni nini kwa Wizara hii ya Kilimo? Kwamba Wizara ya Kilimo ijikite katika mito na kutengeneza *scheme* namna ya umwagiliaji ili wananchi na wakulima walio wengi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waweze kupata mtiririko wa umwagiliaji ili waweze kutoka kwenye gunia tano mpaka kumi waende kwenye gunia 30 mpaka gunia 40 na huu ushahidi ninao katika Jimbo langu la Karatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali katika Wizara hii ya Kilimo; waache kufungua mipaka ya nchi hii kwa muda, waweze kuacha mipaka kwa miezi yote 12 ili

wakulima hawa waweze kwenda kutafuta soko kwenye maeneo mengine nje ya nchi hii ili waweze kufaidi kilimo wanacholima kwa shida, kwa jasho, wasiendeleo kuambiwa kwamba sasa hawawezi kuuza mazao haya ndani ya nchi hii ya Tanzania wakati huo Serikali haijandaa mpango mzuri wa kununua mazao ya wakulima, na wakati huo kama naweza kupata soko kule Kenya na nikaweza kuuza gunia kwa shilingi 200,000 kwa nini Serikali ndani ya nchi hii ya Tanzania wasiweze kununua gunia kwa hiyo shilingi 200,000 ambayo mimi mkulima naweza kupeleka mazao yangu katika nchi jirani ya Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeshaonekana mara nyingi magari ya watu yakitaifishwa katika mipaka ya Namanga, Kilimanjaro na maeneo mengi sana ya nchi hii kwamba sasa wakati huo mpaka ukifungwa unaweza kukosa gari yako au unaweza ukakosa mazao yako, wakati huo Serikali ikidai ndani ya nchi hii kuna upungufu wa chakula. Mimi naamini siyo kazi ya mkulima wa Tanzania kulisha wananchi wa Tanzania, ni kazi ya Serikali kulisha Watanzania na kujua kwamba chakula kinatosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika Wizara ya Maji; katika Jimbo langu la Karatu kuna Mradi wa *World Bank* ambao una takribani miaka kumi sasa haujaweza kukamilika. Lakini vilevile najua kuna Naibu Waziri wa Maji mwezi wa 12 aliweza kutembelea Jimbo la Karatu wakati huo Jimbo hilo la Karatu kuna mradi wa maji yeye alivyokuja mradi uliweza kutoa maji, lakini baada yayeye kuondoka mradi ule haujaweza kutoa tena maji. Lakini vilevile mradi wa aina hii uko kwenye Kijiji cha Getamo, uko Uambang, uko Endanyewe, uko Buger na Khusumai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika eneo la *TRA* Wabunge wengi waliongea; katika Jimbo langu la Karatu *TRA* wameweza kushindwana na wafanyabiashara walio wengi kwa sababu Jimbo la Karatu asilimia kubwa liko kwenye suala la kiutalii. Lakini vilevile hawa watu wa *TRA* kwa Jimbo la Karatu wamekwenda mbali zaidi, wamekwenda kuwahoji wakulima wa Tarafa ya Eyasi na mimi nikiwepo,

kwamba utengeneze mehesabu ya miaka mitatu iliyopita ili uweze kutengeneza hesabu na kuwapelekea watu wa *TRA*. Sasa kwa Jimbo langu la Karatu inaonekana kwamba hawa watu wa *TRA* wamekwenda sasa mbali zaidi kwenda kuwahoji wakulima wanaolima kitunguu katika Tarafa ya Eyasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Twaha Mmpembenwe atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Bahati Ndimbo ajiandae.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuweza kuchangia, lakini kama ulivyonukuu katika mazungumzao yako kama kauli ambazo zinazagaa zagaa kwenye mitandao ni za sahihi mimi sina budi kusema *Innalillahi-Wainnailayhi Rajiuun*, sisi kwake ndiko tulikotoka na huko ndiko tutakaporejea. Lakini ukumbuko wa uhalisia tu ni kwamba Waarabu wana msemu mmoja unasema; sisi binadamu ni *almayyitul-hayyii* (ni maiti ambazo zinatemebea). Kwa hiyo, mimi na wewe na wengine tuliopo hapa wote tujiandae tu na safari hii ambayo mwenzetu kama ni kweli taarifa hizo zitathibitishwa yeye ameshatangulia na sisi tutamfuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba tu niseme kwamba naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Rashid Shangazi.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye hoja iliyoko mbele ya Bunge letu tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wananizonga nyuma hapa, lakini naomba niendeleo kwa sababu kama ulivyotueleza kama Kiti kwamba mamlaka zitatoa taarifa

rasmi, sasa naomba Waheshimiwa Wabunge tuvumiliane kwa sababu mamlaka hizi zinatoka kwake na lazima tuziheshimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma mpango ambao unatuelekeza mpango wa mwaka mmoja lakini pia mpango wa miaka mitano na ninaomba nitoe mchango wangu katika eneo dogo la sekta ya afya, hasa kwenye eneo zima la uwekezaji katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge awamu iliyopita nikiwa Mjumbe katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali tulitembelea *Medical Stores Department (MSD)* na kuona namna ambavyo wanafanyakazi, lakini wakati tuko pale kukawa na *delegation* kutoka nchi za *SADC* ambayo imekuja kufanya uchunguzi ili kuweza kuwapa *MSD* jukumu la kusambaza dawa katika nchi 16 za Kusini mwa Afrika (*SADC*), lakini tulijiridhisha kwamba kwa Sheria ya Uanzishwaji wa *MSD* walikuwa hawana mamlaka ya kuzalisha dawa isipokuwa ni kununua na kusambaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimeleta hoja hii? Nimeleta kwa sababu dawa za binadamu zinazozalishwa hapa nchini ni asilimia nne peke yake katika dawa asilimia 100 ambazo tunazitumia. Ni asilimia nne tu ya dawa ndiyo zinazalishwa nchini; dawa nyingine zote tunazinunua kutoka nje ama Ujerumani au India.

Sasa hoja yangu ni kwamba Wizara inayohusika na uwekezaji ni wakati mwafaka sasa kuhakikisha kwamba inavutia wawekezaji katika sekta hii ya dawa za binadamu ili kama tutapata soko la usambazaji wa dawa katika *SADC* dawa hizi ziwe zinatoka hapa hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Wizara ya Afya iweze kuleta muswada Bungeni wa kuweza kubadilisha sheria iliyoanzisha Mamlaka ya *MSD* ili sasa iweze kuzalisha, lakini pia kusambaza kwa maana kwamba dawa zikiwa zinazalishwa hapa nchini itakuwa rahisi hata kuzisambaza katika hizi nchi za *SADC* tuweze kupata uwezo wa kwamba dawa zitakuwa zinazalishwa ndani ya nchi, lakini

pia kwa kuwa *MSD* inaweza ikawa ndiyo msambazaji katika nchi za Kusini mwa Afrika basi tukapata *multiplier effect* kwenye uchumi wetu kwa mana ya uzalishaji na usambazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo lingine ambalo ninataka kuchangia ni eneo la bandari; kwamba bandari yetu ni *hub* ya kiuchumi kwa nchi za Kusini mwa Afrika. Tunaomba iendelee kuboreshwa kwa maana kwamba kuweza kushindana na bandari nyingine zilizoko Kusini mwa Afrika hasa ile ya Beira na ya Johannesburg, Cape Town lakini pia na bandari ya kule Angola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanini nazungumza hivi? Ni kwa sababu sisi tuko katika Ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo tunakumbana na changamoto za *protocol* mbalimbali za Afrika Mashariki, lakini wakati mwingine hizi *protocol* hazigusi Kusini mwa Afrika. Kwa hiyo, ni lazima tuwe makini sana pindi tunaposaini *protocol* za Ukanda wa Bahari wa Afrika Mashariki, tuzingatie kwamba sisi soko letu kubwa tumelielekeza Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine na la mwisho ambalo ninapenda kutoa mchango ni eneo la viwanja vya ndege; gharama za kutuana gharama za ku-*park* katika viwanja vyetu vya ndege bado ni kubwa. Kwahiyoiili kuwezesha mamlaka hizi za viwanja tuweze kupokea ndege nyingi kwa wakati mmoja, ni lazima tutazame eneo hili la Mamlaka za Viwanja vya Ndege kwa maana ya *landing fees* na *parking fees* ili ziweze kushawishi ndege za mashirika mbalimbali kuweza kutua hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nakushukuru kwa nafasi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Mipango imekamilisha kazi zake kwa sasa.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Kama nilivyokuwa nimewajulisha hapo awali nitampisha Mheshimiwa Spika aje atoe taarifa.

Hapa Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mtakuwa mnafahamu kwamba Mheshimiwa *Engineer* Atashasta Justus Nditiye alipata ajali Jumatano, tarehe 10 Februari, 2021 eneo na Nane Nane hapa Dodoma na kupelekwa Hospitali ya Mkoa wa Dodoma ambayo tumezoea kuiita *General Hospital* kwa matibabu ya awali na baadae akahamishiwa Hospitali ya Benjamin Mkapa pia ya hapa hapa Dodoma ambapo amekuwa akiendelea na matibabu.

Kwa masikitiko makubwa nichukue fursa hii kuwataarifu kwamba Mbunge mwenzetu Mheshimiwa *Engineer* Atashasta Justus Nditiye, amefariki leo Ijumaa, tarehe 12 Februari, 2021 saa nne asubuhi Hospitalini Benjamin Mkapa alipokuwa akipata matibabu.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 173 ambayo inataka kuahirishwa shughuli za Bunge kunapotokea kifo cha Mbunge wakati Bunge likiwa kwenye shughuli zake. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho, Jumamosi tarehe 13 Februari, 2021 saa 03:00 asubuhi ili Waheshimiwa Wabunge tupate muda wa maombolezo.

Taarifa zaidi kuhusu namna tutakavyomuaga Mbunge mwenzetu zitatolewa baadae na *immediately* baada ya hapa naomba Wajumbe wa Kamati ya Uongozi wote hapa kwenye Ukumbi wa Spika nyuma, *Speaker's Lounge*.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa 03:00 asubuhi.

(Saa 05:36 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi, Tarehe 13 Februari, 2021, Saa Tatu Asubuhi)